AGOSTI MMXXIV-TOLEO LA XXXV

# NGURUMO

*ya mwandishi*

Ezenia S. Kamana
'Rey Stanley'
1988-2024
R.I.P



**Fumba macho, lala, pumzika!**

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Fumba macho, lala, pumzika! —Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Twaha Omary Yusuph — Uk 03

**New In Town: —** Operesheni Kasmir, Shangwe — uk 04

**PITIO LA VITABU**— DIWANI YA KIMBUNGA '7'—Uk 06

**MAKALA — SAIKOLOJIA**: …………….—Uk 06 na 07

**MAKALA:** Kitabu Shangwe na Matumaini Mapya ya Hedhi Salama**—**uk 08

**MIAMBA WA AFRIKA:** Muammar Gaddafi '10'— Uk 10

**Sako kwa Bako–** Rebeca W. Kitomari—MTI WA FARAJA **—**Uk 11

**RIWAYA:** — SHAJARA YA MUUAJI '6'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '17'**-** Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 '13- Uk 16

**HABARI:** – Uk 17

**ANDIKO MAALUM:** Fumba Macho. Lala, Pumzika —Uk 18—20

**MALENGA WA KILEO:** Ni Pigo!, Fumba macho — Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Maisha ni Mapambano '4'-Uk 23

**ELIMU JAMII:** — Ukamataji, aupekuzi na Dhamana ya Polisi '7' — Uk 24 na 25

**HADITHI:** Rais wa Chuo '2'— Uk. 26—29

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## TAHARIRI:

# Fumba macho, lala, pumzika!

Naandika kwa kalamu iliyojaa sikitiko!
Salamu zangu zikufikieni popote mlipo Tanzania na nje yake.

Tupo kwenye toleo letu la 35, mwezi huu wa Agosti, 2024. Huu ni mwezi uliyobeba sikitiko kuu katika familia hii ya Jamvi la Simulizi baada ya kuondokewa na mwanzilishi mwenza wa jarida hili pamoja na NGO ya Kitabu Maisha.

Habari hii nzito ilikuwa kama wingu nene, jeusi lenye kila dalili ya mvua isiyokuwepo. Siku ya tarehe 19 Agosti tulipokea taarifa iliyotutia simanzi juu ya mpendwa wetu Rey Stanley na siku tatu kama si nne baadae, asubuhi tulipokea taarifa ya kifo chake.

Tuna majonzi na hatuna la zaidi!

Endelea kuburudika na jarida ulipendalo!

Richard Mwambe
CEO Jamvi la Simulizi.

# MWANDISHI WETU:
# TWAHA OMARY YUSUPH 'SPIDER'

**Toleo la 35 linatua kwa mwandishi huyu utayemsoma. Twaha Omary Yusuph au mwite 'Spider'. Mimi ni nani basi nianze kuzungumza kuhusu yeye ilhali mwenyewe yupo?**

**Lengo mojawapo la jarida hili ni kuwaweka hadharani waandishi unaowajua na usiowajua ili uwasome na uwajue vyema na uwaunge mkono katika harakati zao. Karibu jamvini, keti nasi!**




Twaha Omary Yusuph ndilo jina langu halisi, jina la utani MICHU au SPIDER, mtandaoni na kwenye uandishi natambulika kama Twahir Yusuph.

Ni Mwandishi, Referee na Fundi umeme wa magari. Awali niliota kuja kuwa mwalimu na mchezaji mpira wa miguu, sikujua ningejigawa vipi, ila hivyo ndivyo vitu vilivyonivutia na kuvipenda zaidi, haswa mchezo wa mpira wa miguu.

Nikakazana kwenye *boli,* nilikuwa naupiga mwingi mno, huenda ni kutokana nilishea nao damu! Ndio, baba yangu alikuwa mwamuzi wa mpira wa miguu Tanzania, kipindi hicho alishastaafu.

Miaka miwili mbele nikawa mwamuzi wa mpira wa miguu Tanzania anaetambulika na shirikisho, hapo tayari naandika, Ila sikuwa mwandishi.

Nilianza(ga) tangu nikiyaishi mahusiano yangu ya kwanza kabisa 2012 nikiwa kidato cha pili Tandika sekondari, niliandika kwa sababu ya mwanamke. Nilimiliki counter book mahususi, humo kulikuwa na hadithi moja ya mapenzi, na makala kemkem za mahaba, zote nikimwandikia ayuni wangu.

2015 nilipoanza kumiliki simu janja, nikawa nazipost zile makala hadharani, mtandaoni. Nilichoficha ni picha ya niliyemkusudia tu, alikuwa mrembo sana kabla hawajaniibia.

Hata baada ya penzi lile kuwa kibidubidu sikuacha kuandika, tayari kalamu ilishaingia kwenye orodha ya starehe zangu, niliandika kwa mapenzi, nikawa nawasoma pia waandishi wa mtandaoni. Hussein Molito akawa *favorite* kwangu, alichokiandika niliona tunaendana..

Mwezi wa sita 2021, nilikutana na mwandishi wa makala mtandaoni, Juma Omary Mussa, alivutiwa na *art* yangu, akanisogeza kwa rafikize wabobevu kwenye uandishi wa makala, waliounda kundi la Story fupi Challenge, na huo ndio ukawa mwanzo wa safari yangu ya kiuandishi.

Mwaka 2023 nikachapa kitabu changu cha kwanza UA LA MWANDISHI, hadi kinatoka. Nizipeleke shukrani zangu za dhati kwa kaka kibonge, MuddyB Mwanaharakati, mshkaji ananidai pa kubwa sana.

Hapo ikawa nimetimiza moja ya matamanio yangu, nilifurahia kuwa mwandishi mwenye kitabu, tena kikichapwa na *Role Model* wangu wa uandishi, Hussein Omary Molito.

Changamoto kubwa ya mwandishi ni soko, haswa kwa sisi chipukizi. Maandishi yanahitaji sana watu, na mtu wa kukupa mkono unyanyuke, je unao?

Kuna wazee wa komenti za moto ukipost kava jipya la hadithi mtandaoni "Hichi mapema tu, uniletee nakala yangu" kikitoka, *yayu,* humuoni.

Nilikuwa mwandishi wa makala, hatimaye sasa naandika hadithi, isingekuwa kukumbwa na maradhi hadi sasa ningekuwa na vitabu vinne sokoni.

UA LA MWANDISHI, HAPPY NEW YEAR, KABLA SIJAFA na MOGARAH.

Ushauri wangu kwa waandishi wenzangu, haswa sisi tunaochipukia, TUSIACHE KUANDIKA, hata Mwenyezimungu hakuiumba Dunia kwa siku moja, *Let's keep it up.*

HAIJAISHA HADI IISHE.

Ili kuzipata kazi zake tembelea facebook akaunt yake: **Twahir Yusuph.**
Au Whatsapp: **0689043436**

## NEW IN TOWN :
## OPERESHENI KASHMIR na SHANGWE

Kitabu hiki kimeandikwa na Richard Mwambe...

'PT - 502 - B. PEGAN X' Ndiyo chanzo cha yote. Mfumo maalum wa usalama uliopachikwa kwenye ndegevita mpya kabisa ya kisasa na ya kwanza Afrika unatikisa matajiri wanaomiliki maisha ya watu na kutengeneza pesa kwa kutoa roho zisizo hatia.

Serikali na Jeshi la Wananchi Tanzania wanafanya manunuzi ya ndegevita tatu zenye mfumo huo hatari wa kujilinda na kung'amua makombora achilia mbali kushambulia.

Lakini ndege hiyo inatekwa na wajuvi huku ndani yake ikiwa na makepteni watatu.

Huku Tanzania, kiza kinene kinatanda juu ya hilo. Vikao haviishi ili kujua hatima ya yote. TSA1 Kamanda Amata anafunga mjadala kwa kuingia msambweni. Anaanzia Dar es salaam, Zanzibar, Islamabad mpaka Kashmir.

Je nini huko kitajiri? Hii hapa OPERESHENI KASHMIR, kalamu ya 'Mmwela' aliyebarikiwa.

**Kitabu hiki kinapatikana**
**Dar es salaam, Duka la Kona ya Riwaya**
**Simu namba 0655248085**





**SHANGWE**

**HEDHI SIO SIRI**

Miongoni mwa changamoto inayokabili jamii yetu kwa ukubwa wake ni kufanya suala la hedhi kuwa Siri.Wazazi/walezi KUSHINDWA kufunguka kuhusu hedhi na kuwaandaa watoto kabla ya umri kufika ili ukifika wasishtuke na kuona ni jambo la ajabu, lakini wengine hata baada ya jambo hilo KUTOKEA Huwa wanashindwa kutoa elimu na kuwasukumia watu wengine ndio watoe elimu hiyo, ambapo hao watu wengine wanaweza kutoa elimu sahihi ama lah. Wengine hufika mbali na kuitumia hiyo nafasi kuwarubuni watoto na kuwafanyia mambo mabaya.
Wengine kwa kukosa elimu sahihi na kuambiwa na watu wasio sahihi wanatumbukia kwenye mabalaa mbalimbali.

Pamoja na mambo mengine kitabu Cha SHANGWE kimeelezea kwa upana usiri wa HEDHI na matokeo yake katika jamii lakini pia kimetoa suluhisho la nini kifanyike kuondosha changamoto hii.

TAREHE 30 MWEZI Huu (Agosti) katika Shule ya Sekondari ya Kibasila, tutakitambulisha kitabu cha SHANGWE, tutatoa elimu ya hedhi salama na kugawa pedi za pacify kwa wanafunzi.
SHANGWE, HEDHI SIO SIRI Ndio *slogan* yetu
Shiriki nasi kuwapa watu shangwe kwa SHILINGI **10,000/=** tu ukinunua kitabu utakua umechangia UNUNUZI WA TAULO za kike kwa wanafunzi wanaoishi kwenye mazingira magumu.




Inawezekana kwa Mimi na wewe kushiriki pamoja.

**0653544133 tigo**
**Mariam Mbano.**

Ukilipia toa taarifa

# KITABU: KIMBUNGA (DIWANI) - 6



***Kutoka toleo lililopita...***

Mwandishi anaieleza jamii umuhimu wa kutoa shukrani pale mtu anapofanyiwa hisani na mtu mwingine. Katika shairi la "Punda" mwandishi ameonesha jinsi baadhi ya watu wasivyo na shukrani kwa wenzao pale wanapotendewa mema. Mwandishi ameonesha kuwa mwandamu asiye na shukrani hata umfanyie wema kiasi gani hawezi kutoa shukrani. Ameelezea kuwa mtu asiye na shukrani ni vyema kuachana naye au kumtenga (kutengana naye) kabisa. Anasema;

*"Punda hakumbuki wema, hata kwa mchunga wake,*

*Humpa mwingi mtama, na maji anufaike,*

*Katu haiwi salama, shukrani zake mateke,*

*Ndiyo tabia ya punda, kurusha rusha mateke,*

*Kuchunga akikushinda, muwachiye ende zake."*

Katika ubeti huu, mwandishi anasisitiza umuhimu wa kutoa shukrani pale tunapofanyiwa fadhila au jambo jema.

**UJUMBE**

Ø Dhana potofu ya kudhani bila ya kuwa na uhakika wa mambo haifai katika jamii kwa sababu hupotosha ukweli wa mambo.

Ø Mapenzi na ndoa ya dhati ni muhimu katika jamii zetu

Ø Ukoloni mamboleo, uongozi mbaya, rushwa na ukosefu wa elimu ni baadhi ya vikwazo vya ujenzi wa jamii mpya hapa nchini.

Ø Maadili mema na maonyo ni njia pekee ya kuiweka jamii katika misingi ya haki na usawa.

**FALSAFA**

Mwandishi anaamini kuwa maadili mema na maonyo ni njia pekee ya kuiweka jamii katika msimamo na mwenendo bora wa maisha na anatetea misingi ya haki na utu katika jamii.

**MSIMAMO**

Msimamo wa mwandishi una hali ya udhanifu kwani amejadili baadhi ya mambo kwa kudhani tu bila kuwa na misingi ya kisayansi.

**FANI**

**a) Muundo**

Mwandishi ametumia miundo tofauti katika diwani hii kama vile;

Ø Tarbia *(mistari 4)* katika shairi la Kisomo cha manufaa,

Ø Tathlitha *(mistari 3)* katika shairi la "Kujitawala" (uk 7-8).


Ø Takhimisa *(sabilia) – mistari 5* na kuendelea katika shairi la "Punda" na shairi la "Bahati".

**b)Mtindo**

Mtindo uliotumika ni ule unaofuata kanuni za kimapokeo yaani urari wa vina na mizani pamoja na mpangilio wa beti. Karibu mashairi yote yana vina vya kati na mwisho isipokuwa katika mashairi ya "Kimbunga","Dumuzi', "Madereva","Chuwi" yana nusu mstari katika kituo.

**c)Matumizi ya Lugha**

Mwandishi ametumia lugha rahisi iliyoshehenezwa lahaja ya Kiunguja yenye mafumbo na taswira mbali mbali pamoja na tamathali za semi kidogo na misemo kwa kiasi.




d) **Tamathali za semi**

**Tashibiha**

Ø Kwenye shairi la "Sifa ya Mke" (uk 40)

· *Ufedhuli na uovu kama yake mazoea.*

· *Awe kama malaika mzuri kupindukiya*

**Tafsida**

Mwandishi ametumia mbinu ya kufumba kwa kusema maneno makali, machafu, matusi kwa kutumia tafsida. Mfano shairi la "Nyang'au" linahusu tamaa, Paka" linahusu wizi, shairi la "Dumuzi" linakemea uvivu,n.k.

Mbinu Nyingine za Kisanaa

***Inaendelea Ukurasa wa 25***

# -SAIKOLOJIA-

## SAIKOLOJIA YA MALEZI

Madame Neema Mgao,

+255 763 013 206.
The Magic Author,
Dodoma,TANZANIA.



Kumekucha tena; siku mpya na mambo mapya. Katika makala ya Saikolojia mwezi huu nimeona tuangazie jambo nyeti sana la malezi kwa watoto na vijana wetu. Naliita nyeti kwa kuwa, msingi wa maisha na tabia za mwanadamu huanza kujengwa tangu utotoni kabisa.

Hakuna mtu anayezaliwa tu na kukua bila kujengewa misingi ya kuishi. Mtoto anapozaliwa hupita katika hatua mbalimbali hadi kufikia utu uzima.
Zipo hatua mbalimbali ambazo wanasaikolojia wengi wamezitanabahisha katika ukuaji wa mtoto, kwamba ni lazima azipitie hatua hizo tena kiukamilifu ili kuweza kukamilisha ule mzunguko wa ukuaji wake bila kuruka hatua hata moja. Mzazi au mlezi unapaswa kushuhudia hatua zote za ukuaji wa mtoto wako.
Tuone hatua za ukuaji wa mtoto.

MWAKA 0-1.
Hii na hatua ya awali kabisa, katika hatua hii mtoto hujifunza kula tu. Katika hatua hii wanasaikolojia wengi wametanabahisha kuwa ni hatua hii ambapo mtoto kila anachoshika yeye hupeleka kinywani.

MIAKA 1-3.
Hapa ni muhimu sana kwani katika hatua hii furaha ya mtoto huwa katika njia ya haja kubwa. Hatua hii ni muhimu sana mzazi akaisimamia vizuri ili mtoto ajue kuwa njia ya haja kubwa ni kwaajili ya kutoa haja kubwa tu. Ni katika hatua hii ambapo mtoto asiposimamiwa vizuri anaweza baadae kuwa muumini wa mapenzi kinyume na maumbile au ushoga. Hapa mtoto anapojinyea usimfokee bali mfundishe kuwa ipo sehemu maalumu kwa ajili ya kufurahia kutoa haja kubwa.

Mtoto asipoifurahia hatua hii, au amejisaidia wewe mzazi au mlezi umemfokea, umempiga, utamfanya airuke hatua hii maana ataikosa ile raha. Na kwakuwa njia ile ina raha na wewe umemzuia mtoto kuipata kwa ukali wako, utamfanya baadae atumbukie kwenye kushiriki mapenzi ya jinsia moja. Na akianza kuingiliwa kinyume na maumbile na kuanza kuihisi ile raha ya kwenye njia ya haja kubwa, basi mtoto au kijana huyu kumbadilisha itagharimu saana. MWACHE MTOTO AFURAHIE KUTOA HAJA KUBWA.

MIAKA 3-5.
Hii ni hatua ambayo tunaweza kusema ndio msingi wa tabia za mwanadamu. Katika umri huu ndio hapa utaona mtoto wa kiume anakua karibu zaidi na mama yake, na mtoto wa kike anakua karibu sana na baba yake. Ndio ule msemo ya kuwa mtoto wa kike anampenda baba yake na wa kiume anampenda mama yake. Ni tabia ambayo kiuhalisia sio nzuri na inamadhara sana hapo baadae.
Wanasaikolojia wengi wanasema kuwa tabia hii isipokemewa mwanzoni kabisa inapomea ndio hapo baadae humfanya kijana apende kukaa katika kundi la wanawake ilihali yeye ni wa kiume, au binti apende kukaa kwenye kundi la wanaume .
Wameenda mbali zaidi na kugundua kuwa hata mavazi hasa upande wa mtoto wa kike anapokua karibu na baba. Wakati baba anawaza kumtengeneza binti awe imara na jasiri basi atajikuta anamzoesha mtoto wa kike kuvaa sana mavazi ya kiume. Sijasema kwamba watoto wasiwe karibu na wazazi wao, la, nachomaanisha ni wazazi kuwa na kiasi katika ukaribu na watoto wao wenye jinsia tofauti na zao.
Tofauti na hivyo, mzazi atajikuta anamtengeneza kijana wa kiume anaedekadeka hovyo kama mama yake, na kijana wa kike anaekua mbabe mbabe kama baba yake.

5 - BALEHE.
Huu ni wakati ambao mwanadamu anakuwa na hisia sana na jinsia tofauti na yeye. Hatua hii huchagizwa au huchochewa na hatua ya 3, kwamba kama mtoto aliachwa awe karibu na baba yake sana basi atakapokuwa katika hatua hii ndio muda atakua anapenda sana kuwa karibu na wanaume. Au mtoto wa kiume kama hakusimamiwa kiukamilifu basi ndio muda ambao asilimia kubwa ya rafiki zake watakua ni rafiki wa kike. Ingawa, jamii inaweza kusema “yule ndivyo alivyo, anapenda marafiki wa kike ilihali yeye ni wa

kiume, au anapenda marafiki wa kiume ilihali yeye ni wa kike". Jamii imechukulia kuwa ni jambo la kawaida ila kiuhalisia kabisa sio jambo zuri.
Hatua hii isiposimamiwa basi ndio tunapata kuona mashoga, au mimba za utotoni. Nasisitiza hatua hii isimamiwe ipasavyo.

BALEHE MPAKA KIFO.
Hapa ndio mwanadamu ameshakamilika sasa, tunampata mwanadamu ambae ndio ameshapitia hatua zile nne zote huko juu. Hapa ndio tunampata mwanadamu kamili kwamba kama alipikwa sawasawa basi jamii itampata muungwana, na kama hakulelewa sawasawa basi ndio jamii itashuhudia kizazi cha hovyo sana.
MZAZI AU MLEZI, ILI KUMPATA MWANADAMU MWENYE MATOKEO CHANYA KATIKA MAISHA YA WATU WENGI, BASI YAKUPASA KUHAKIKISHA HATUA ZILE 4 ZA MUHIMU UMEZIFANYA KIUKAMILIFU ILI USIJE KUTULETEA KITUKO KATIKA JAMII.
Jamii hivi sasa inashuhudia mmomonyoko wa maadili kwa vijana wetu. Mmomonyoko huu umekua ni wa kiwango kikubwa saana katika miaka ya hivi karibuni kutokana na uchagizwaji wa mambo kadha wa kadha, tuone baadhi ya mambo hayo:-

A]. MALEZI MABOVU.
Katika hatua ya 4, ama hatua ya balehe, hapa wazazi wengi hufanya makosa sana. Ile hali ya urafiki kupitiliza kwa mtoto wakidhani kuwa wanafanya vizuri kumbe ndio wanakosea. Mama anamsimulia mtoto wake wa kike mwenye miaka 22 pengine, anamsimulia namna anavyotongozwa na vijana, au baba anapomsimulia kijana wake wa kiume namna alivyolala na binti fulani wa mitandaoni au binti wa mtaani.

NINI KINAZALISHWA AKILINI MWA VIJANA HAWA WAWILI WALIO NA URAFIKI KUPITILIZA KWA WAZAZI AU WALEZI WAO?.
Kinachozalishwa ni dharau kwa wazazi wao. Mtoto wa kike kwanza hatomuheshimu huyo mama  na pia kisaikolojia hatomuheshimu baba yake, kwa maana ataona kuwa baba ameshindwa kumdhibiti mama mpaka anatongozwa na vijana wadogo. Na vivyo hivyo kwa mtoto wa kiume, hatomuheshimu baba yake. Ndio!  Baba si amemfanya mtoto kuwa msiri wake! Mtoto hatomuheshimu baba na pia ataona kuwa mama ameshindwa kucheza nafasi yake kumdhibiti baba mpaka baba anatoka na mabinti *mtaa wa nne*. Hii itapelekea dharau hata kwa wababa au kwa wamama wengine. Ndio itapelekea mtoto wa kike kuwa na mahusiano na wanaume wanaomzidi umri. Kwakuwa ameshamdharau baba yake kule nyumbani, vipi wa mwenzie atamheshimu? Itapelekea pia mtoto wa kiume kuona kuwa ni kawaida na hatoumia atakapoanzisha mahusiano na wanawake wenye umri sawa na mama yake. Hii ni kwa sababu ile ile, ameshamdharau mama yake hivyo hatoona kama kuna ubaya kuwa na mahusiano na mmama. Wenyewe wanakauli pendwa ya kilaana kuwa UMRI NI NAMBA. Wazazi na walezi ndio wa kulaumiwa kwa kusababisha mmomonyoko huu mkubwa sana wa maadili.

"NICHUKUE NAFASI HII KUTOA POLE KWA FAMILIA  YA MWASISI MWENZA WA JARIDA LA NGURUMO YA MWANDISHI KUFUATIA KUONDOKEWA NA MPENDWA WETU BI. EZANIA KAMANA *[REY STANLEY]*. MUNGU AMPE PUMZIKO LA MILELE MPENDWA WETU.

RAHA YA MILELE UMPE EEH BWANA,NA MWANGA WA MILELE UMUANGAZIE, APUMZIKE KWA AMANI, AMINA.

Kwa leo tuishie hapa,hadi wakati mwingine tena Mungu akipenda tutaangazia sababu nyinginezo pia. Kwa ushauri kuhusiana na maswala ya ndoa, malezi, mahusiano na maisha kwa ujumla wasiliana na mimi kwa whats'app no.+255 746 139 654, au nipigie simu kupitia +255 763 013 206.

The Magic Author,
Madame Neema Mgao,
Dodoma,TANZANIA.

# KITABU SHANGWE NA MATUMAINI MAPYA YA HEDHI SALAMA

SHANGWE ni simulizi iliyoandikwa kwa ushirikiano wa waandishi watatu, ambao ni Mohammed Hammie, Mariam Mbano na Hamisi Kibari, wote wakiwa washindi wa tuzo mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Hii ni simulizi inayomhusu msichana anayeanzisha harakati za hedhi salama shuleni baada ya kupitia magumu kadhaa.

Wazo la kuandika simulizi hii limetokana na binti aitwaye Johan Hoppness. Msichana huyu aliwahi kuanzisha harakati za hedhi salama katika Shule ya Sekondari ya Ilkiding'a iliyopo mkoani Arusha mwaka 2021 hadi 2023 alipohitimu Kidato cha Nne. Johan ni zao la mradi wa kitabu kilichoandikwa na Mohammed Hammie cha Maji Mandiga.

Kwenye kitabu hiki mhusika mkuu ni msichana tuliyempa jina la SHANGWE. SHANGWE anawakilisha kundi kubwa la wasichana ambao wanapitia changamoto za kupata hedhi salama kutokana na kukosa maarifa ya suala hili la asili kufanywa siri kutokana na baadhi ya imani za mila na tamaduni zetu.

Tofauti na imani iliyopo kuwa wasichana hawawezi kujipambania dhidi ya matatizo yao, SHANGWE anathubutu na kuwaonesha upande wa pili kuwa inawezekana msichana kupaza sauti na kupigania anachokiamini hadi kujikomboa.

Kwa sababu hali ya hedhi iliyomtokea ilikuwa ngeni maishani mwake, Shangwe alianza harakati za kusaka ukweli. Alipoujua, ndipo alipoanza kuyasaka maarifa sahihi. Misukosuko, fedheha, vitisho na hatari alizokutana nazo havikuwa kikwazo kuleta SHANGWE kwa wasichana wanzake waliopitia changamoto ya hedhi salama.

Mapito yake kwenye simulizi hii yanatoa nafasi ya kuwafanya wasichana wengine kujijengea ujasiri wa kujiamini, kuthubutu na kuchukua hatua hasa wanapokuwa kizani. Lengo ni kuhakikisha wakati wa hedhi wanakuwa salama na kuhudhuria masomo yao kwa mustakabali wa ustawi wa maendeleo yao ya baadae. Waandishi wa kitabu hiki wanaamini kuwa ikiwa simulizi hii itawafikia wasichana wengi nchini, waalimu na hata wazazi Tanzania basi itakuwa ni ukombozi mkubwa kwao na jamii kwa ujumla katika kujitambua hasa linapokuja suala la hedhi na hedhi salama.

Kitabu cha SHANGWE kimekuja wakati mwafaka ambapo utafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ulionesha ukosefu wa vyumba vya kujisitiri kwa wanafunzi wa kike wakati wa hedhi shuleni, umefanya baadhi yao kutumia vichaka.
Pia umebaini asilimia 60 ya wasichana kushindwa kumudu gharama za ununuzi wa taulo za kike, hivyo kutumia vifaa visivyo salama kiafya.

Utafiti huo uliofanyika mwaka 2021, uliwahusisha wasichana takribani 10,516,801 katika shule 294 kwenye mikioa 16 kote nchini.

Pia kwa mujibu wa Wizara ya Afya Tanzania, takwimu zinaonesha kuwa hapa nchini wanawake na wasichana zaidi ya milioni 13, wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49 hupata hedhi kila mwaka. Na idadi hii ni kubwa, hivyo jamii ina kila sababu ya kuhakikisha kuwa kundi hili linapata huduma bora wakati wa hedhi ikiwemo kuhakikisha uwepo wa maji, sabuni na taulo za kike ili kufanya hedhi iwe salama kwao.
Huu ni msukumo mwingine uliofanya muunganiko wa waandishi wa kitabu cha SHANGWE wakae chini na kuandika simulizi inayounga mkono jitihada za serikali kwa kutumia fasihi andishi ili kuhakikisha jamii inapata elimu ya hedhi salama.

“Hedhi sio balaa, sio siri, sio ugonjwa na wala sio laana bali ni mabadiliko ya hali ya kawaida yanayomtokea mwanamke au msichana mara baada ya kupevuka” aliwahi kusema aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (Mb).

Kitabu cha SHANGWE kimethibitishwa lugha na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) hivyo kinaweza kusomwa na watu wa kila rika. Kitabu kimetunukiwa cheti nambari BKT/ITH/25/24.

Jalada ya kitabu cha SHANGWE limechorwa na Chris Katembo ambaye ni

mchoraji wa siku nyingi wa kujitegemea. Ni mchoraji wa katuni na vielelezo vya vitabu kwa takribani miaka 25 sasa.

Kimehaririwa na Ndugu Jonathan Ngua, yeye ni afisa elimu katika Kaunti ya Kilifi nchini Kenya. Ana shahada ya ualimu (BAED) katika Chuo Kikuu cha Mount Kenya. Pia ni mwalimu, mtunzi na mhariri wa kazi za fasihi ya Kiswahili.

Kitabu cha SHANGWE kinachotoka leo (Agosti 30) kina timu kubwa iliyokizunguka. Nyuma ya posters zote yupo mtu makini Ndugu Kizito Mpangala ili kuhakikisha kazi inakuwa ya viwango.

Waandishi wa kitabu cha SHANGWE wanatabaruku kitabu hiki kwa wasichana na wanawake wote ulimwenguni ambao wanapitia madhila na misukosuko ya kukosa hedhi salama na pia kugubikwa na maisha ya mila na utamaduni uliopitwa na wakati katika jamii zao kuhusu hedhi, hasa wasichana wadogo shuleni ambao mara nyingi wamenyimwa fursa kuijua elimu ya hedhi.

**60% ya wasichana kushindwa kumudu gharama za ununuzi wa taulo za kike, kumewafanya watumievifaa visivyo salama**








**Muamar Muhammad Abu Minyar Al - Gadafi**

Inaendelea...

Wafuasi walipongeza utawala wa Gaddafi kwa kuunda jamii yenye usawa kupitia marekebisho ya ndani. Walisisitiza mafanikio ya serikali katika kupambana na ukosefu wa makazi, kuhakikisha upatikanaji wa chakula na maji salama ya kunywa, na maboresho makubwa katika elimu. Wafuasi pia walipongeza mafanikio katika huduma za afya, wakisifu huduma za afya bure kwa wote zilizoandaliwa chini ya utawala wa Gaddafi, ambapo magonjwa kama kipindupindu na homa ya matumbo yalidhibitiwa na maisha ya watu yalizidi kuwa bora.

Matibabu ya serikali ya Gaddafi kwa Walybia wasio wa Kiarabu yalipata ukosoaji kutoka kwa wapigania haki za binadamu, ambapo Waberber wa asili, Wataliani, Wayahudi, wakimbizi, na wafanyakazi wa kigeni walikumbana na mateso katika Libya ya Gaddafi. Vikundi vya haki za binadamu pia vilikosoa matibabu ya wahamiaji, ikiwa ni pamoja na wale wanaotafuta hifadhi, ambao walitumia Libya ya Gaddafi kama njia ya kuelekea Ulaya. Wakati wa Vita vya Kiraia, vikundi mbalimbali vya mlengo wa kushoto viliunga mkono waasi wanaompinga Gaddafi—lakini si uvamizi wa kijeshi wa Magharibi—kwa kudai kwamba Gaddafi alikuwa mshirika wa ukoloni wa Magharibi kwa kushirikiana na Vita dhidi ya Ugaidi na juhudi za kuzuia uhamiaji wa Kiafrika kuelekea Ulaya. Gaddafi alionekana kama mhalifu wa kigaidi, hasa nchini Marekani na Uingereza.

## TATHMINI BAADA YA KIFO

Mijadala ya kimataifa kuhusu kifo cha Gaddafi iligawanyika. Gaddafi alichukuliwa kama shujaa na wengi katika Afrika ya Kusini mwa jangwa la Sahara, lakini alikemewa kwa upana katika sehemu nyingine.

Baada ya kushindwa katika vita vya kiraia, mfumo wa utawala wa Gaddafi uliporomoshwa na kubadilishwa na serikali ya mpito ya NTC, ambayo ilihalalisha vyama vya wafanyakazi na uhuru wa vyombo vya habari. Mnamo Januari 2013, GNC ilibadili rasmi jina la Jamahiriyah kuwa "Nchi ya Libya." Wafuasi wa Gaddafi kisha walianzisha chama kipya cha kisiasa, Front ya Watu kwa Ajili ya Uhuru wa Libya. Kiongozi wa chama hicho, Saif al-Islam Gaddafi, aliruhusiwa kushiriki katika uchaguzi mkuu ujao.

Tukutane toleo lijalo, Je ni nani Mwamba wa Afrika atakuwa kwenye safu?



Kaburi la Muamar Gaddafi


# SAKO KWA BAKO:

## REBECA WILFRED KITOMARI: Mti wa Faraja

**Katika toleo la 34, ndani ya safu hii ya Sako kwa Bako tulikuwa na mwanadada huyu mrembo, Rebeca Kitomari. Tulizungumza naye mengi sana lakini tulisema kuwa bado katika toleo lifuatalo ana jambo la kutueleza.**

**Rebeca… katika mahojiano yetu yaliyopita ulituambia kuwa "wataka watu watambue siri iliyojificha kwenye vitabu…" nimesikiasikia kwa rafiki zako wa karibu kuwa umechapa kitabu, hebu tuambie juu ya kitabu hicho…**

Mti wa Faraja ni kitabu cha hadithi kilichoandikwa nami, kikilenga watoto wenye umri wa miaka mitano na kuendelea. Hadithi hii inamhusu Faraja, mtoto jasiri mwenye upendo wa dhati kwa bibi yake. Baada ya bibi yake kuugua, Faraja anaamua kwenda msituni kutafuta dawa, na katika safari hiyo, anakutana na changamoto ya kupambana na nyoka hatari, lakini kwa ujasiri wake, anafanikiwa kumshinda na kuleta dawa kwa bibi yake.




Kwa kutambua umuhimu wa upatikanaji wa tiba kwa urahisi siku za usoni, Faraja anapanda mti wa dawa nyumbani kwa bibi yake, ambao baadaye unakuwa msaada mkubwa kwa jamii nzima. Kwa kuthamini juhudi za Faraja, wanajamii wanaupa mti huo jina rasmi la Mti wa Faraja. wakionesha jinsi juhudi za mtu mmoja zinavyoweza kuleta mabadiliko chanya kwa jamii nzima.

**Asante kwa melezo. Kitabu hiki kinalenga nini, tuambie…**

Kitabu hiki kinalenga kukuza maarifa ya utunzaji wa mazingira na mbinu mbalimbali za kujikinga na dharura na majanga, huku kikiweka mkazo kwenye ushirikiano wa jamii katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

**Unaamini vipi katika hilo?**

Mimi ninaamini kuwa watoto ni wapokeaji na wasambazaji wazuri wa maarifa. Kupitia hadithi hii, watoto watafundishwa umuhimu wa kupanda miti kama sehemu ya utunzaji wa mazingira na kuchukua tahadhari za mapema ili kuepuka athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, watoto hawa wanatarajiwa kuwa mabalozi wazuri wa kile watakachojifunza kutoka kwenye hadithi hii.

**Ulipataje wazo la kuandika kitabu hiki?**

Wazo la kuandika kitabu hiki lilizaliwa kutokana na dhamira yangu ya kuelimisha jamii kuhusu majanga na dharura mbalimbali, pamoja na mbinu za kukabiliana na majanga hayo. Njia mojawapo niliyoona inafaa zaidi ni kupitia vitabu vya hadithi, hasa kwa watoto. Watoto wanapenda hadithi, na wao ni mabalozi wazuri wa maarifa, hivyo, wanapopata elimu, jamii nayo inaelimika.

**nikitazama kitabu hiki, naona mambo makubwa matatu yanayoijenga taswira ya ndani ya mwandishi, nikimaanisha kuwa mwandishi anaweza kuwa a)mwalimu b)mwanamazingira c)mhudumu wa afya.... je ukweli wako uko wapi kati ya haya matatu? yaani wewe ni nani?**

Mimi ni mwalimu niliyesomea Fasihi na Jiografia chuo kikuu cha Dodoma (UDOM). Masomo haya yamechangia sana katika kuandaa kitabu hiki. Pia, nimesoma elimu ya majanga, na maarifa niliyopata katika kozi hii yamenichochea kutaka kujifunza zaidi kuhusu elimu ya majanga. Hivi sasa, nasoma shahada yangu ya pili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambako utafiti wangu unalenga hasa masuala ya elimu ya majanga katika taasisi za elimu.

**wasomaji wangependa kujua kama kitabu hiki kitapatikanaje kwa wale ambao watahitaji....**

Kitabu Mti wa Faraja kinatarajiwa kuwa tayari mwezi Oktoba. Kwa wale watakaohitaji nakala ya kitabu hiki, wanaweza kuwasiliana na mwandishi, Rebeca Wilfred Kitomari, kupitia namba yake ya simu +255743031109.

**Asante sana Rebeca na tunakutakia yote mema!**

# SHAJARA YA MUUAJI—6

Na. Richard Mwambe



***Inatoka toleo lililopita...***

**Alikuwa muuza maji maarufu sana kuanzia Tandika Sokoni mpaka Davis Corner na Kona ya bandari kwenda Mwembeyanga. Alisifiwa kwa upole, uaminifu na uchapakazi. Maisha yake alijaribu kuyaweka kiudaresalamu lakini hali yake haikukubali.**

***Endelea...***

Kipato cha siku kilikuwa ni wastani wa shilingi elfu sita. Alikotoka aliacha wazazi wasiojiweza, wadogo zake wakisoma na kadhalika. Wateja wake wakubwa wa maji walikuwa wakinamama hasa wale waliokwishaolewa na walikuwa wakihitaji huduma hiyo kwa hali na mali. Hata kama angepita muuza maji mwingine wasingenunua, walimtaka Magena Makange. Alikuwa na wateja wa oda maalum ambao kila siku lazima apeleke maji na kuna wale wa kawaida ambao wakikuona ndipo watanunua.

Huduma yake, labda, ndiyo iliyowafanya wanawake hao wapende kununua maji kwake tu. Atawasili na mkokoteni wake, atakuongelesha kidogo, mtacheka. Kisha atakubebea madumu mawili mawili kukupelekea mpaka ndani huku we mwenyewe ama una mfuata nyuma au yeye akufuate nyuma. Madumu mawili ya mwisho ndiyo yalikuwa na utata, akiingia ndani kwako atachelewa kutoka, inaweza ikachukua dakika kumi na tano mpaka ishirini. Baada ya hapo ataondoka zake mpaka wakati mwingine.

Alizoeleka, kwani alikuwa mtaani hapo kwa takribani miaka minne, muhamiaji kutoka Ikizu.

❦

Akiwa kajiegemeza pale ukutani simu yake ndogo iliyofungwa kwa rababendi ikaita. Akaitoa kwenye mfuko wake wa jinzi na kuitazama. Ijapokuwa kioo chake kilifubaa lakini yeye aliweza kusoma jina la mpigaji. *'Malikia wa nguvu'* ilijiandika.
Magena akatabasamu, *Malkia* alikuwa akimpigia. Hakusita. Aliiweka sikioni baada ya kubonyeza kwa shida ile batani iliyotumbukia ndani.
Kilochomshitua zaidi ni sauti ya kiume iliyosikika upande wa pili.

*"Ninaongea na Magena Makange?"* Ikamuuliza.
"Ndi-ndi-nddddiyo Mimi..." Akajibu kwa kutetemeka akajua wazi kuwa simu hiyo haina wema.
*"Hapa ni kituo cha polisi Chang'ombe, kuna mtu yuko hapa anaitwa Aziza unamfahamu?"* Akaulizwa.
"Ndiyo namfahamu!"
*"Ana shida na wewe na anahitaji msaada wako, uje Mara moja!"*
"As-sa-sawa afande!" Akajibu.
Magena akajikuta kama aliyepigwa sindano ya ganzi. Ni kweli, anamfahamu Aziza. *Kuna nini?* Akajiuliza. Akajiangalia alivyo, miguuni alikuwa na kandambili za *umoja*, suruali yake ya jinzi na jezi yake ya timu Manchester ya enzi na enzi iliyochoka kwa jasho kutokana na hali yake 'kauka n'kuvae'.

*Aziza amefanya nini?* Akajiuliza. *Na kwanini wanipigie Mimi, Nina msaada gani?* Maswali yote hayo hayakuwa na majibu. Magena akarudi mpaka mahali alipopanga huko Maguruwe na kuacha mkokoteni wake. Tayari ilikuwa saa kumi na moja ikikaribia kumi na mbili jioni. Akaondoka zake kwa mguu kuelekea kituoni huku mapigo ya moyo wake yakienda bila mpangilio maalum.

Alipofika kituoni alipokelewa na afande aliyekuwa kaunta. Alipojitambulisha, moja kwa moja alifikishwa katika ofisi ya upelelezi ambamo ndani yake alikuwamo afande Damasi aliyeshikilia kesi hiyo. Magena alikaribishwa kiti. Aliketi akiwa anatetemeka kwa hofu. Polisi ni polisi tu!
"Habari bwana Magena Makange!" Damasi alimsabahi huku macho yake ya kiaskari yakimtalii. Ilikuwa ni vigumu sana kwa askari huyo kijana kukubaliana na mawazo yake kwamba Magena aliyemtaka ni huyo. *Anaweza kuwa anafahamiana na Aziza huyu au namba zimeingiliana tu?* Akajiuliza. Mbele ya Damasi aliketi Magena Makange, kijana kwenye siha njema lakini mwili wake ulifubaa kwa shida, mavazi yake yaliusawili ufukara wake. Nywele hazikupitwa na chanuo. Harufu ya jasho nayo ilikuwa dhahiri shahiri.
"Nje-njema ..." Akajibu.
"Unafahamiana na Aziza?" Akamuuliza ili kuweka mawazo yake sawa, ajue kama anawaza sawa au la.
"Ndi-ndiyo..."
"Mnafahamiana vipi?"
"Ni rafffiki yangu..."
"Mara ya mwisho umemuona wapi au mlikutana wapi?" Damasi akauliza akiwa kayakaza macho yake. Ukimya kidogo ukatawala.

Mawazo kadhaa yakazunguka kichwani mwa Magena. Aseme asiseme? Vipi kama ni mtego na anayemuuliza katumwa na mume wa Aziza au huyo askari ndiye mume

wa Aziza au bwana wake na ana tetesi zake. Mawazo yakamchefua. *Aliniambia hana mume wala bwana!* Akajifariji.
"Usiku wa kuamkia leo!" Akajibu.
"Wapi?"
"Mibingiriko gesti hausi!" Magena akajibu.
"Mh!" Damasi akaguna na kumtazama askari mwenzake, PC aliyekuwa kando. Labda aliguna kwa kuwa, kwa hali ya kijana huyo na kwenda gest kukutana na Aziza havina uhusiano.
"Ulionana na Aziza?" Akamuuliza.
"Ndiyo afande! Nilionana naye?" Akajibu.
"Enhe... Kwa kuwa wewe ni rafiki yake, unaweza kutuambia Aziza yuko wapi?" Damasi akauliza.
Magena akabaki kimya, hana jibu.
"Tujibu!!!" Damasi akasema kwa sauti ya kushtukiza iliyomfanya Magena almanusura aanguke.
"A-a-anaweza kuwa Morogoro!"
"Umejuaje?"
"Alinambia ana safari ya Morogoro asubuhi ya Leo..."
"We uliachana naye saa ngapi?"
"Saa kumi na moja afande!"
"Kwa hiyo masaa matatu ulikuwa na mke wa mtu gesti?" Damasi akauliza kwa ukali.
"Sa-sa-sa-maahani braza, a-a-likuwa ananiitaga mwe-mwenyewe!" Magena akajibu huku akilia.

Damasi akajiegemeza kitini.
"Afande! Mlete Ujoro..." Damasi akamwagiza yule askari mwingine.
Haikuchukua muda, askari wa kike akaingia pale ofisini akiwa kamtanguliza Ujoro mbele. Ujoro akaoneshwa mahali pa kusimama, akafanya hivyo. Kila Mara alikuwa akipiga miyayo ya njaa. Huruma!
"Ujoro!" Damasi akaita.
"Bee!" Ujoro akaitika kwa sauti ya chini iliyojaa njaa na uchovu.
"Unamjua huyu kijana?" Akamuuliza.
"Ndiyo namjua..."
"Unamjuaje?"
"Mara nyingi huja pale gesti hasa Aziza akiwepo!" Ujoro akajibu.
"Mara ya mwisho ulimwona wapi?" Damasi akauliza.
"Usiku wa jana, alikuja kama kawaida yake kwa Aziza," Ujoro akaeleza.
"Na alipoondoka ulimwona?"
"Hapana, sikumwona..." Ujoro akajibu.

Tsh 4000/= Softcopy. Lipia Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Whatsapp 0766974865

Damasi akamtazama Magena, akatikisa kichwa kushoto kulia. *Hivi Aziza alikuwa anakosa nini hadi kulala na mwanaume kama huyu?* Akajiuliza.
"Ujoro, nikisema kuwa Magena Makange ndiye aliyemuua Aziza... Utakubali utakataa?"
Sentensi hiyo ilimshitua Magena, akajikuta amesimama kwa wahka, "amekufa? Nani kamuua? Aaaaaaaa!" Magena akaangusha kilio cha nguvu.
Inspekta Msaidizi wa polisi, Damasi, na yeye akasimama.
"Ndiyo, ameuawa, na wewe ndiye mtu wa mwisho kuwa naye na hata ulipotoka pale gesti ulipitia mlango wa siri. Huyu ni mhudumu hakukuona," Damas akaongea kimamlaka.
"Hahahahahapana afande ... Mi-mi-mi ssssijaua afande!" Magena Akalia kwa uchungu. Magena Makange alijawa na woga na kupelekea hata majibu yake kuwa ya woga vilevile. Si kwamba hakujua hali ya Aziza bali aliona kwa kusema moja kwa moja inaweza kumletea shida. Akadanganya.
"Hayo yote utayajibu mahakamani!" Damasi akamaliza kazi yake na kuamuru Magena kuwekwa lupango. Alipobaki peke yake, akaketi na kuiinamia meza yake. Tayari ilikwishafika saa moja na nusu za jioni. Damasi alikuwa amechoka sana maana Siku hiyo hakupata hata muda wa kupumzika. Akaitazama picha ya mwili wa Aziza uliokuwa umelala katika sakafu ya chumba cha gesti nusu uchi. *Hii ndiyo shida ya kujiokotea wanaume msiowajua mwisho wenu ndo kama hivi!* Akaiambia ile picha kwa sauti ya moyoni mwake.
*Aziza, ulikosa nini mpaka unatembea na kijana huyu mchafu asiyejua sabuni? Ona sasa uzuri wako wote umeishia mochwari!* Akaendelea kunung'unika kana kwamba marehemu alikuwa mkewe au bibi yake. Damasi bado alikuwa hajaamini kama Magena alikuwa mpenzi wa siri wa Aziza maana walikuwa watu wa madaraja tofauti.
***Itaendelea...***

***Kutoka toleo lililopita***

"Samahani dada, kuna hii bahasha niliichukua hapa, lakini nimegundua kuwa si yangu, nilipewa kimakosa, sasa nimeirudisha na naomba samahani kwa hilo," akamkabidhi naye akaichukua na kuiangalia kisha akaitia chini ya meza.

***Endelea...***

"Asante maana hii kitu ilitunyima raha, imeleta mgogoro mkubwa sana na mabosi," yule mwanadada akaeleza. Baada ya hapo wakaagana na Amata akatoka katika ofisi ile na kuingia garini akaketi tena.

Mara hii alikuwa na namba ya Carlos ambayo ameichukua pale kwa mlinzi. *Nitampigia!* Akawaza na kuondoa gari eneo lile, akaagana na wale wazee na kutimkia mjini.
Hakupoteza muda kwa kwenda mbali aliegesha gari lake jirani kabisa na baa kubwa, kandokando tu na barabara ile iliyosheheni malori ya mizigo. Juu ya duka hilo kulikuwa na maandishi yanayowakawaka yakisomeka 'SHIMO LA UDONGO LUXURY PUB'

❦

Watu walijazana katika pub hiyo wakiselebuka muziki wa Msondo. Kamanda Amata akaweka pembeni tu gari lake. Hakuteremka, ila akashusha kioo na kuyatupa nje macho yake. Vurugu zilizokuwa nje zilitosha kumjulisha kuwa huko hakukuwa kukipitika. Mbele ya gari lake walionekana akinadada kama watatu hivi waliokuwa wamevaa kiajabuajabu kiasi kwamba ilitosha kuonekana kuwa walikuwa kwenye biashara.

"Kssssss!" akaita kwa mtindo huo ambao kwa vyovyote ungewafanya wageuke, na ndivyo ilivyokuwa. Akampiga mkono mmojawao, naye akasogea bila shida.

"Karibu, karibu kaka jisikie nyumbani, cha fasta elfu tano, usiku mzima elfu thelathini…"

"Asante!" Amata alijibu huku mkononi mwake ikining'inia noti ya shilingi elfu kumi, "sikia, nahitaji bia moja baridi sana.

Hakikisha unapenyapenya unaniletea hapa, chenji baki nayo," akamwambia. Yule mwanadada hakuamini, maana tangu afike hapo hakukamata *buzi* lolote la kuchuna lakini mara hii akajikuta akipata bahati ya mtende. Wakati mwanadada yule kapotelea huko baa, Amata akachukua simu ya Marietha na kuipiga kwake akapata kuijua namba ya mwanadada huyo. Na mara hiyo akachukua simu yake akapiga kwa Chiba.

*"Yes kaka, unasomeka bila shida…"*

"Kazi moja tafadhali…" akamwambia.

*"Waiting…"*

"Nataka nyavu nina samaki wa kuvua jioni hii…"


*"Nipe uelekeo …"* Chiba akamjibu Amata naye akatuma namba za simu anayotaka kuipigia na ile atakayotumia kupiga.

*"Copy,"* akamaliza na kukata simu.

Kioo cha gari kikagongwa, Amata akakishusha taratibu na kumwona yule mwanadada akiwa tayari na kinywaji kile mkononi. Akakipokea na kukitazama, kilikuwa hakijafunguliwa.

"Asante sana," akashukuru.

"Asante na wewe, ukimaliza utanishtua nirudishe chupa," yule mwanadada akaondoka na Amata akapandisha kioo kwa mara nyingine. Kabla hajapiga simu ile anayoitaka akafungua ile bia na




kupoza koo. Funda moja la nguvu likaisha na nusu ya bia katika chupa ile. Akaitua na kuiweka mahali salama.

Baada ya kubonyeza tarakimu anazozitaka katika simu hiyo ya Marietha, akaiweka sikioni kusubiri kusikia nani ataitikia.

*"Hello!"* sauti ya kike ikaitikia.

Amata hakujibu akaendelea kusikiliza sauti ile kwa minajiri ya kuitambua kama ni ya kiume ila imebadilishwa tu au ni ya kike halisi. Ijapokuwa alikuwa amezituliza fahamu zake lakini bado hakuweza kugundua siri iliyojificha katika sauti hiyo.

"Samahani, nina shida na Bwana Carlos, yupo?" akauliza.

*"Carlos? Ndiyo nani huyo, mbona simjui?"* ile sauti ikauliza.

"Ok, wrong number, sorry!" Amata akajibu kumaanisha kuwa amekosea hiyo namba, akakata simu.

Dakika moja baadae, simu yake ikaita, alipoichungulia alikuwa Chiba.

"Yes bro'…!"

"Msasani, karibu na Mayfair Plaza," Chiba akamwelekeza.

*"Ok, fanya hivi, mweke kwenye signal kisha unicheki nikifika ili nimpate vyema,"* Amata akamwambia Chiba.

"Na jina lake hapa linaonesha ni Mrs. Honduras Kenston, inaonekana siyo Mtanzania huyu!" Chiba akaongeza.

"*Copy! On the move now*," akajibu na kuinua ile chupa akaimwagia kinywani na kuimaliza, akawasha gari na yule mwanadada akasogea mwenyewe.

"Asante sana kwa ukarimu wako," akampa ile chupa.

"Oooh jamani, mbona bado sijakuonesha ukarimu, nipe japo dakika tano tu nikuoneshe wa Kiafrika," yule mwanadada alibembeleza huku akilegeza macho yake.

Kamanda Amata hakutikisika, kwa kuwa alielewa kuwa mwanadada huyo yupo katika kutafuta riziki ijapokuwa si kwa njia halali.

"Usijali, siku nyingine nitakuja, leo nimebanwa kidogo, *by the way* jina lako nani?"

"Tatu Athuman!"

"Ok!" akamjibu na kuchukua namba zake za simu, kisha akaondoka eneo hilo na kuelekea Msasani.

**08**
**NIGERIA**
**Hoteli ya Benizia**

MIRABEL alikuwa juu ya kitanda kikubwa ndani ya chumba cha hoteli hiyo ambacho Codec alipanga kwa saa hizo atakazokuwa hapo Onitsha. Pamoja na kujigalagaza kote hapo kitandani, Mirabel hakuona hata dalili za tamaa ya ngono kwa mwanaume huyo. *Labda hii haimvutii!* Aliwaza na kubadilisha mtindo wa mlalo; mara ajigeuze hivi mara ajibinue vile. Codec alikuwa kama anayetazama sinema katika ukumbi. Hakushtuka, wala moyo wake haukudunda. Katika meza iliyokuwa mbele yake, kulikuwa na chupa kubwa ya pombe kali. Aliendelea kunywa taratibu.

"Ric, njoo tulale mpenzi, njoo nikupe mambo ya Ki-naijaa," Mirabel alibembeleza huku akijitadua nguo zake za mwisho zilizobaki mwilini.

"Subiri, kuna jambo nataka nilimalize, kisha tutapeana raha," akajibu na kujimiminia kinywaji kinywani mwake akasubiri kidogo kumeza ili apige funda lingine.

"Kwa nini umekuja Nigeria?" akauliza Mirabel na sentensi hiyo ikamfanya Codec kushusha bilauri iliyokuwa tayari kwenda kinywani.

"Si nimekwambia mi ni mtalii," akamjibu. Wakati huo, Mirabel alichukua mkoba wake na kumwaga vitu vilivyomo, kisha akawa anavipekuapekua pale kitandani. Jicho la Codec likatua kwenye kidubwasha kimoja kidogo mfano wa heleni, akainuka haraka alipo na kukinyakua. Mirabel akauwahi mkono wa Codec lakini tayari ulikuwa umeshaondolewa eneo lile na mtu mzima huyo keshaketi kitini kama mwanzo. Akakitazama kile kidude na kisha akamtazama Mirabel.

"Wewe ni mpelelezi? Unanipeleleza sio?" akauliza Codec huku jicho limemuwiva kwa hasira.

"Hapana, mi si mpelelezi," Mirabel akajibu.

"Si mpelelezi, hiki ni nini?" akamwuliza huku akimwonesha ile heleni. Mirabel akabaki kimya bila kujibu kitu. Codec akatikisa kichwa juu chini. *Kumbe!* Akawaza kisha akamvamia Mirabel, "utaniambia leo!" akang'aka na kumzaba makofi mawili mazito. Mirabel akaangukia kitandani.

"Niambie, unamfanyia kazi nani?" akamwuliza tena huku akiwa kamkandamiza pale kitandani.

"Hapana, mi-mi siyo m-pe-le-lezi," akajibu huku akilia kwa uchungu.

"Sasa wewe ni nani na hiki kitu cha nini?" akamwuliza.

"Su-bi-ri, n'takwa-mbi-a…"

❦

*"He is here,"* kijana mmoja akamwambia mwenzake kuwa yupo hapo.

"Yap, sasa bosi kasema amalizwe, tutumie mbinu gani, tumvamie hotelini au?" akauliza mwingine.

"Anamtaka kama alivyo, tena anawataka wote kwa sababu Mirabel kuna kipindi alizima kinasa sauti chake tukawa hatujui alipo, hili ni kosa tena kosa kubwa," aliyekaa kiti cha nyuma kwenye gari hilo akawaambia wenzake.

*"Ok, let's go!"* akawaambia wenzake waende na wote wakateremka kwenye lile gari.

Wakavuta hatua na kuingia katika hoteli ile. Hakuna aliyewauliza lolote kwa kuwa vijana wa Mathis hawakuwa wageni machoni pa raia wa Nigeria hasa katika mji huo. Wakapanda ngazi kama kwao na kuufikia mlango walioelekezwa.

Pigo moja la nguvu mlango ule ukaachia na kubaki wazi.

***Itaendelea...***

Yule mwizi akampa mkono wa salamu Mustafa na kumuonesha sarafu ya dhahabu.

"Najua uliwahi kushona suti ya marehemu fulani katika nyumba moja hapa mjini." Alisema yule mwizi. "na jana ulimpeleka rafiki yangu katika hiyo nyumba, na kaweka alama ya chaki katika mlango ili asiweze kuipoteza katika kumbukumbu yake. Lakini kwa bahati mbaya kuna mtu aligundua hiyo alama na kuweka alama kama hiyo katika kila mlango wa nyumba, hivyo tumeshindwa kuifahamu. Naomba unipeleke katika hiyo nyumba uliyoshona suti ya marehemu, lakini, mimi nitaweka alama ya chaki nyekundu kwenye fremu ya dirisha, alama hiyo itakuwa ndogo sana kiasi ambacho hakuna yeyote atakayeweza kuiona.

Mustafa akaiangalia ile sarafu ya dhahabu. "Ukinilipa vizuri, nitakupeleka." Alisema.

"Nitakulipa vizuri." Mwizi alimjibu. "lakini utavaa kitambaa machoni kama ulivyofanya mwanzo."

Mwizi akachukua kitambaa chekundu na kumfunga nacho Mustafa machoni na kisha wakaanza safari.

Baada ya muda mfupi, Mustafa akasimama na kuvuta harufu. "samaki!" Mustafa alisema. "napenda sana harufu ya samaki akipikwa! Mke wangu huwa ananipikia samaki kila Jumamosi. Hapa lazima tukate kushoto."

Dakika chache baadaye, akasema Mustafa. "Huyo mbwa anabweka! Nafikiri ana njaa na anataka chakula chake cha jioni. Tuifuate hiyo sauti kisha tutakata kulia."

Kisha tena baadaye kidogo akasema, "Naukumbuka huu muziki, kuna mtu huwa anapenda sana kuchezea zumari na filimbi maeneo haya kama nilivyosikia mara ya kwanza. Nafikiri tunakaribia kufika."

Mwishowe kabisa kwa mshangao, "Waridi! Oooh! Napenda sana harufu ya haya maua, na hapa nina uhakika ndipo kwenye hiyo nyumba, tumeshafika."

Harufu ya maua hayo yalikuwa yakitoka kupitia kwenye dirisha moja la nyumba ya Kassim. Hiyo ndiyo nyumba ambayo Alibaba, mkewe, mtoto wake, mke wa Kassim pamoja na mfanyakazi wao Marjane walikuwa wakiishi.

"Ahsante sana!" alisema Yule mwizi. "umenifanyia kazi nzuri sana mzee wangu." Kisha akampa sarafu zaidi za dhahabu.

Mwizi alitabasamu huku akienda kwenye dirisha la nyumba hiyo na kuweka alama ndogo sana ya chaki nyekundu kwenye fremu ya dirisha hilo.

"Hakuna mtu atagundua alama hii ndogo sana," alijisemea mwizi. "Kiongozi atanifurahia sana!" Kisha akamrudisha Mustafa kwenye kibanda chake cha kushonea nguo naye akarudi kuelekea msituni.

❦

Jioni ile, Marjane alikuwa akiandaa chakula cha jioni kwa aajili ya familia ya Alibaba na wenzake nyumbani. Aliandaa nyama ya kuku, kachumbari na mchanganyiko wa mbogamboga mbalimbali, alipomaliza kuandaa mchuzi ule wa kuku na mbogamboga akaanza kuandaa upishi wa wali, alichukua sufuria na kuweka maji kiasi, kisha akaweka sufuria hiyo kwenye jiko. Baada ya hapo aliendа mpaka stoo kuchukua mchele ili aweze kuchambua na kuusafisha kabla ya kuutosa kwenye maji, kwa bahati mbaya sasa, akakuta mchele hakuna.

"Itabidi tu niende kununua mchele" alijisemea moyoni. Marjane akachukua kapu lake la sokoni na kuelekea mjini sokoni.

Alipokuwa akirudi aliona alama ndogo nyekundu kwenye fremu ya dirisha, macho ya Marjane yalikuwa mazuri sana, hakuwa na matatizo ya macho hata kidogo.

"Hii alama haikuwa hapa kabla" Marjane alijisemea moyoni. "Mara ya kwanza alama nyeupe, na mara hii tena alama nyekundu!! Vizuri sana! Nitafanya kama nilivyofanya mara ya kwanza."

Aliingia ndani na kwenda kuchukua chaki nyekundu. Kisha akarudi nje na kuweka alama nyekundu katika kila fremu ya dirisha kwenye nyumba zote za mtaa ule.



## SHANGWE YAIPAMBA KIBASILA

Na Mwandishi wetu

Shule ya Sekondari Kibasila, jana (30/8/2024) ilikipokea Shangwe kwa shangwe. Hii ni mara ya pili kukitambulisha kitabu cha SHANGWE. Meneja wa mradi huo Bi. Mariam Mbano anasisitiza kuwa 'hakijazinduliwa bado ila kwa sasa lengo ni kuwapa fursa wadau kukipata na kukisoma. Uzinduzi huenda ukafanyika mwakani kwenye siku ya hedhi'.

Pamoja na yote hayo, bado balaa lake sio mchezo. Siku ya jana cheche zilitoka katika Shule ya Sekondari ya Kibasila. Vijana wa leo wanasema 'ilikuwa ni full shangwe'.

Katika tukio hilo la kukitambulisha Shangwe, nakala za kitabu hicho ziligawiwa bure. Pamoja na hilo, wanafunzi wa kike walipatiwa sodo (pedi) bure. Washiriki walipendezeshwa kwa fulana za Shangwe. Wimbo maalum wa Shangwe ulipigwa mbashara na kukifanya Shangwe kuwa shangwe kweli. Siku hiyo elimu ya hedhi salama ilitolewa kwa vijana. Waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali walialikwa na kuipa siku hiyo uzito wa aina yake. Mmoja wa waandishi wa kitabu hicho, kilichoandikwa na waandishi watatu anataja jambo hilo kuwa ni 'Maana halisi ya "Writing with Purpose"'.



**Wakiwa makini na wenye furaha wakifuatilia mafunzo ya Hedhi Salama.**

## Je; Shangwe ni mtoto wa Mandiga?

Ufanikishwaji wa mradi huu wa kitabu cha Shangwe umetiwa mkono na WCWSA OKIA - Our Kids In Africa Sun Fresh Water, LLC COMFY CARE12, Pacify, Tanzania MHH Coalition, Vogic China Supply, Women and Children Welfare Support Association (WCWSA), Afri-Glow International na The game changers team.

Mmoja wa washiriki maalum Bi. Joyce Maketa amewataka wazazi kuichukulia hedhi salama kama sehemu ya huduma ya msingi kwa mtoto wa kike. Pamoja na wote pia Balozi wa Pacify Bi. Elizabeth Michael (Lulu) alishiriki katika kugawa sodo hizo jambo lililowapa *amsha amsha* wanafunzi hao kwa kumuona nyota huyo wa filamu nchini.



**Bi. Mariam Mbano (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wawakilishi wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kibasila.**



**Katika kila kitabu, kuna kurasa za mwanzo, kati na mwisho. Hebu tufungue kurasa za kati, lakini zile za karibu na mwishoni...**

MWEZI Agosti mwaka huu, ni mwezi uliobeba simanzi nzito katika jiji la Dar es salaam na vitongoji vyake hususani Tandika Maghorofani. Ukurasa wa mwisho wa kitabu cha maisha ya rafiki yetu Rey Stanley ulizua taharuki kubwa na kuacha hali ya sintofahamu miongoni mwa waliomjua ama kwa jina tu au kwa kukutana naye. Mengi yamezungumzwa, mengi yameandikwa na mengi yamesemwa lakini ukweli ni kwamba mpendwa wetu Rey amepumzika katika usingizi wake wa milele. Kitabu kimefungwa!

Hebu sasa tufungue ukurasa mwingine wa nyuma kabla ya huu wa hatima yake. Tujue maisha yake katika muktadha wa kifasihi, mahusiano yake na Amata Ric. Huu ni ukurasa wa dhahabu ambao wengi wetu hatukuwahi kuujua. Haya ni maneno au majibu kutoka kwa Amata Ric kufuatia maswali mengi yaliyoulizwa na watu kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii na inbox zake anazotumia.

“Mtu mmoja aliniuliza… ‘Ulikuwa unamtag mara nyingi kwenye post zako, Rey alikuwa mkeo?’ swali hili lilijitokeza mara kadhaa kule inbox, basi napenda kukujibuni hivi…


Rey Stanley hakuwa mke wangu. Mahusiano yangu na yeye yalijengwa katika muktadha wa vitabu. Alipojua kuwa mimi ni mwandishi wa vitabu tena simulizi zile anazozipenda, alipenda kuwa mmoja wa wadau wa jukwaa la jamvi la simulizi. Kwa kuwa mimi ninaishi mbali na jiji hili kubwa la Dar tofauti na yeye basi niliona ni jambo zuri kumjumuisha katika harakati zangu ili awe msaada. Ni kweli Rey alikuwa msaada mkubwa sana katika shughuli nzima ya maswala ya vitabu na fasihi katika jukwaa letu.

Ngoja niwasimulie kidogo simulizi hii tamu…
Tarehe 25/08/2018 ndiyo tarehe ambayo mimi na marehemu tuliketi meza moja kwa mazungumzo mazito. Moja ya mazungumzo hayo ilikuwa ni kuhusu Jamvi la Simulizi. Rey aliniuliza maswali saba ambayo majibu yake niligundua kuwa anayo yeye mwenyewe kuliko mimi.

Alilijua Jamvi la Simulizi tangu 2015, lakini 2018 kwa maswali yake ndipo nilijuwa kuwa ana jambo analopenda kufanya kwenye Jamvi. Nikampa nafasi. Mwaka 2019 kilipochapwa kitabu cha MPATANISHI. Aliniambia, ‘**Ric *Mpatanishi ni kizuri sana, ngoja ni-study jambo nitakwambia…’*** nikamwambia ‘sawa’. Sikujua nini anafanya. Nilipokuwa namtuma huku na kule kufuatilia hili na lile na yeye alikuwa anafanya utafiti wake wa siri.

Aliporidhika na utafiti wake, siku moja tulikuwa tumeketi karibu na nyumbani kwao akaniambia tena, ***‘simulizi yako ya Operesheni Kashimir ni nzuri ajabu…’*** nami nikamwambia nafikiri kuichapa kitabu, akakataa. Akasema ***‘usichape kitabu, uza nakala laini,’*** sikukataa. Nilikubali na kuanza kuuza nakala laini. Naweza kusema wazi kabisa kuwa kama kuna simulizi imeingiza pesa nyingi kwa nakala laini basi ni Operesheni Kashmir, kwa rekodi aliyokuwa akiihifadhi yeye mwenyewe kwenye *notebook* yake.

Baada ya hapo akaniambia ***‘Chapa hiki Harufu ya Kifo’***. Wakati anasema hayo, mimi nilikuwa nipo vibaya kiuchumi. Nakumbuka, nakumbuka sana,



alisema ***‘lazima tuchape’***. Rey alichukua mkopo wa 800,000 ili kutimiza wazo lake. Katika uzalishaji wa

Kitabu Harufu ya Kifo kila kitu alisimamia mwenyewe. Awamu ya kwanza ya vitabu alisimamia mwenyewe mauzo tena ya mkono kwa mkono. Ilikuwa ukitaka kitabu ufuate nyumbani kwao au atakuletea na alifanikisha.

Ndani ya miezi mitatu, alifanikiwa kurudisha ule mkopo na riba yake japo aliuomba kwa miezi sita. kisha ndipo kitabu kile kikaingia dukani na kwa mawakala.

Rey alipenda sana misemo niliyokuwa naiandika kwenye simulizi. Na misemo mingi hii alikuwa anapenda kuiandika kwenye *Whatsapp status* zake. Mfano wa msemo mmoja wapo ambao Rey aliupenda sana na aliurudia mara nyingi kuutamka ni huu **"Kamwe marehemu hawezi kuuona msalaba wa kaburi lake…",** msemo huu upo kwenye simulizi ya GENGE.

Siku ya mazishi yake pale Kinondoni nilikumbuka sana huu msemo, nililia machozi. Nilikumbuka mengi, mengi sana.

**Je, utamuenzi katika moja ya vitabu vyako?** Hili lilikuwa swali la msomaji wangu mmoja aliyeniuliza inbox, nalijibu hapa.

Ndiyo! Nitamuenzi, naweza kukwambia tu kuwa tayari simulizi ipo na imekamilika ambayo imemuenzi. Nilishaiandika, na simulizi hii ilikuwaje nikaiandika? Ni yeye mwenyewe ndiye alitoa wazo. Aliniambia, ***'andika simulizi moja, tumia jina langu kama mhusika…'*** nilishaiandika na yeye ameshaisoma, na aliifurahia sana. Sasa si tu mhusika kuwa na jina lake na tunu ya kitabu nitampa yeye kama mmoja wa mashujaa wa Jamvi la Simulizi. Nitamuenzi kwa simulizi hiyo ambayo nitatangaza lini ujio wake ila itakuwa 2025.

Majuma mawili kabla ya kufunga kitabu cha Rey nilihojiwa na Tungo Tata TV (ya mtandaoni). Moja ya kitu nilichokizungumza ilikuwa ni kuhusu Jarida hili la Ngurumo ya Mwandishi kwamba ni Rey Stanley ndiye aliweka jina la jarida hili. Nilimshirikisha wazo kuwa nataka kuwa na kitu ambacho wapenzi wa fasihi Tanzania na nje yake watakuwa wakipata habari, makala, taarifa na simulizi kwa njia ya jarida pepe. Haraka akaniambia, ***'nilishawahi kufikiri hilo, basi fanya moja tuone linafananaje…'*** nikaanda na pamoja na majina manne ambayo nilitaka achague moja ambalo litabeba uhalisia wa jarida lenyewe. Akayasoma na kunijibu '…***aaaa bwana hii ni Ngurumo ya Mwandishi'*** basi jarida hili likaitwa jina hilo. Na mwanzoni yeye alikuwa ndiye anayefanya *proof reading* kabla hatujalitoa.
Hakuishia hapo, daima alikuwa anasapoti mawazo yangu, na kunipa mambo mapya kama naweza kuyafanyia kazi. Mwaka 2022 mimi na yeye na rafiki wachache tukaja na wazo la kuwa na NGO itakayojikita katika maswala ya usomaji wa vitabu. Nilipoweka wazo lile mezani (tulikuwa sita) yeye akawa wa kwanza kusema ***'litakuwa jambo zuri'*** na mara moja akajiteua kuwa katibu. Michakato ikaanza na mpaka inafika wakati wa kusajiri, wengine walishakata tamaa tukabaki watatu; mimi nikiwa Mkurugenzi, yeye Rey katibu wa kujiteua na mwingine mratibu.

Haikuwa rahisi, mpaka tunafikia kusajili, tulibaki wawili wengine walikuwepo kama vivuli hawakuwa na sapoti. Mwaka 2023 tukafanikiwa kusajiri NGO ya KITABU MAISHA. Wakati sasa ndiyo shirika linataka kuanza kazi rasmi, na tulikuwa tumeandaa warsha ya usomaji wa vitabu kule Iringa, Rey Stanley akaniacha, akaondoka kurudi kwa Muumba wake. Sikutegemea, wala sikuwa tayari. Na bado ni ngumu sana kwangu kukubaliana na ukweli. Kila mara natazama namba yake ya simu labda ataniandikia chochote cha kunitania au kazi kama kawaida yake.



Ni pigo!

Mambo ambayo wewe ulikuwa huyajui kuhusu Rey ni haya; Rey ni mtoto wa nne katika familia ya watoto sita. Ametuachia watoto watatu; wa kike wawili na wa kiume mmoja.

Alikuwa mtaalam sana na mwalimu wa kutengeneza batiki *(tie and die),* sabuni za kusafisha vyombo, nguo na sakafu zenye manukato ya aina aina. Alijua kuongea, na daima aliupasua ukweli pale inapobidi, alikuwa na kipaji cha asili cha uandishi.

Amewahi kufanya kazi mara kadhaa na Taasisi ya FASDO yenye ofisi zake pale Tandika Maghorofani pia amesimamia mradi wa NURU uliyopo hapohapo Tandika Maghorofani kwa kipindi cha muda mfupi lakini kwa mafanikio makubwa. Alikuwa ni mwanamke anayeweza kukupa matokeo mazuri na makubwa kama ukijua nafasi ya kumpa.

Mpaka kitabu cha maisha yake kinafikia tamati, Rey alikuwa Katibu wa Jumuia ya Wazazi ya CCM tawi la Maguruwe, Tandika. Alikubalika sana na aliowaongoza alijitahidi sana kutatua migogoro iliyoshindikana. Na hii yote aliiweza kwa kuwa alikuwa msikivu kutoka kwa mimi mshauri wake. Nilipomuuliza mara moja anataka nini kwenye siasa, alinijibu ***'nataka niijenge Tandika mpya ya CCM'.*** Lakini mpaka anaondoka bado alikuwa akipambania ndoto zake. Inasikitisha!



Tunatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki. Tulimpenda lakini Muumba amempenda zaidi. Yote juu ya yote tumuombee kwa Mola: amsamehe makosa yake, ampokee Mbinguni na aketi naye kwenye utukufu wa utakatifu wake.

Naweka kalamu chini nikimwambia rafiki yangu huyu…

Fumba macho, lala, pumzika! Nakupenda sana! Na nitakupenda daima!

Pumzika kwa amani...

**Picha ya familia mbele ya kaburi la mpendwa wetu Ezenia S. Kamana (Rey Stanley)**




**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

**NI PIGO!**

Ni pigo limetukuta, pande zote Maanani
Syamini lilomkuta, mpendwa wetu hanuni
Hata kama tutaputa, tutaempiga ni nani
Ni pigo lenye uchungu, kwetu na kwa familia

Ni ngumu kuvumilia, inaporudi kichwani
Twazidi kumlilia, Rey wa maghorofani
Pole kwenu familia, na nyote mlo shakani
Ni pigo lenye uchungu, kwetu na kwa familia.

Chozi linanidondoka, mimi Shujaa Maneno
Kwanini umeondoka, bila kutwachia neno
Hakika hutofutika, kwa mawazo na maneno
Ni pigo lenye uchungu, kwetu na kwa familia

Mkono watetemeka, kwandika hili shairi
Moyo wangu wateseka, kila nikitafakari
Hasira yayonifuka, juu ya huyo jahiri
Ni pigo lenye uchungu, kwetu na kwa familia

Ni pigo lenye uchungu, kwetu na kwa familia
Hakimu wetu ni Mungu, sote tunamlilia
Wa duniani na mbingu, yeye tunamuachia
Ni pigo lenye uchungu, kwetu na kwa familia

Natoa salamu zangu, za pole kwa ndugu wote
Najua mna uchungu, na pia kwa sisi sote
Naomba tumwache Mungu, awe hakimu wa yote
Ni pigo lenye uchungu, kwetu na kwa familia

Tuzidi kumuombea, peponi awe hakika
Apumzike kwa Jalia, Baba alo Mtukuka
Nasi tuliyobakia, bado tutakukumbuka
Ni pigo lenye uchungu, kwetu na kwa familia

**Na. Shujaa Maneno**
**Bagamoyo—Pwani.**
**24/8/2024**

**Fumba macho, lala, pumzika!**

Ni neno gani niseme kukukumbuka?
Ni wimbo gani niimbe kukukumbuka?
Ni shairi gani nighani kukukumbuka?
Ni simulizi gani nisimulie kukukumbuka?

Ni kinywaji gani ninywe kukukumbuka?
Ni chakula gani nile kukukumbuka?
Ni picha gani niiangalie kukukumbuka?
Ni mkoa gani niende kukukumbuka?

Kwa nguo gani nitakukumbuka?
Kwa msuko gani nitakukumbuka?
Kwa mwendo gani nitakukumbuka?
Kwa jambo gani nitakukumbuka?

Fumba macho, usiutazame ulimwengu
Fumba macho, yote mwachie Mungu
Fumba macho, samehe kwa nchi na mbingu

Lala, usingiziwo mkuu
Lala, usingizi usio makuu
Lala, miguuni pa mwenye ukuu
Lala, utaamshwa na parapanda kuu

Pumzika, yaache ya mlimwengu
Pumzika, mikononi mwa Mungu

Pumzika, pumzika Rey!

**Na. Richard Mwambe (Amata Ric)**
**Dar es salaam —Tanzania**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# Habari Picha




PICHA:

Tukio la kutangza Pedi za Pacify, kilikuwepo pia kitabu kipya kabisa cha SHANGWE.

Marm’z Relationship Hub… kama kawaida iliwasilisha kitabu kipya cha SHANGWE kilicho-andikwa na waandishi watatu.

Elizabeth Michael Lulu aliteuliwa kuwa balozi wa Pacify Pads nchini.

Picha zote zilipigwa siku ya tukio.

Picha ya duara: Mariam Mbano (Mkurugenzi wa Marm’z), Mr. Luvanda (Katibu), Dr. Naytham (Mdau wa karibu) waki-furahia jambo.






# KUTOKA MAKTABA: MAISHA NI MAPAMBANO—3

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

**SURA YA PILI**

TAMAA YA UTAJIRI WA HARAKA HARAKA

Mpepo, baada ya kusimulia juu ya mkasa wa maisha yake, ambayo yalijaa visa na mikasa alieleza jinsi alivyokumbwa na wimbi la utajiri wa haraka haraka.

Siku moja, majira ya mchana, Luzolo rafiki yake, alifika nyumbani kwake kumshawishi:

Luzolo: Ndugu Mpepo sahiba yangu, nina jambo ambalo ningependa kukwambia.

Mpepo: Niambie kwanza, huna haja ya kuniarifu. Wewe ndiyo mimi na mimi ndiyo wewe nadhani unafahamu hivyo.

Luzolo: Kweli kabisa. Habari yenyewe inahusu kujinasua na ufukara. Nimepata mawazo mapya kuhusu jambo hili.

Mpepo: Sema tu rafiki yangu, ni habari njema zipi hizo.

Baada ya hapo Luzolo alimweleza rafiki yake kwa kirefu kuhusu mipango yake. Mipango ilihusu uchimbaji wa madini mkoani Rukwa. Alimwambia kwamba vijana wengi wametajirika sana kwa kazi hiyo: wengine wana maduka makubwa, mabasi ya abiria, mashine za kusaga nafaka na hata kufanya biashara na nchi za nje kwa kutumia makontena!

Mpepo kusikia hivyo, alivutiwa sana na kuanza kumdadisi mbinu watakazotumia hadi kufika huko na kuanza kazi ya uchimbaji madini.

Mpepo: Je, hakuna matatizo? Kwanza vifaa tutapata wapi?

Luzolo: Hakuna tabu. Tutapanda magari ya kawaida. Kwanza pale Mkuze sehemu yenye madini ni karibu na Tunduma. Pia kuna watu ni naowafahamu. Vifaa vya kuchimbia ni sururu, jembe, sepetu na karai la kuzolea mchanga.

Mpepo: Kama nilivyosema hapo awali kweli hizi ni habari njema. Hata mimi nilikuwa sipati usingizi kwa kubakia katika hali hii. Ni kweli kabisa watu wengi wamepiga hatua. Baadhi yao ni watumishi wa serikalini, katika mashirika, makampuni na hata wale wasiofahamika shughuli zao ni nini wanaishi maisha matukufu. Nadhani hakuna haja ya kupoteza muda; wazo tayari, iliyobaki ni utekelezaji. Si unajua usemi kwamba 'Ajizi nyumba ya njaa!'

Luzolo: Tuondoke kesho au keshokutwa inafaa zaidi?

Mpepo: Bila shaka.

Luzolo: Haya mimi naondoka. Keshokutwa Jumamosi tutaondoka. Kama hatukupatwa na mkasa wowote tutafika Tunduma Jumapili saa za alasiri; hatimaye Mkuze.

Mpepo: Tunduma siyo Zambia? Naogopa kuvuka mipaka ya nchi, hasa nikikumbuka mateso ya siku za nyuma.

Luzolo: Sawa, Tunduma ni Zambia vile vile ni Tanzania—ina pande mbili kama vile Mlima Kilimanjaro au Namanga kule Arusha.

Mpepo: Kama ni hivyo sawa. Jumamosi saa kumi na mbili alfajiri nitakuwa mlangoni.

Siku ya Jumamosi iliwadia. Mpepo aliamka mapema sana. Akamwamsha Sofi, mke wake. Kabla hajamweleza lolote Tabu akaanza kulia—maana hajazoea kuachwa peke yake kitandani majira kama yale. Hivyo Sofi akabaki kitandani amelala huku akimkumbatia Tabu. Sofi akamuuliza Mpepo.

Sofi: Kwani unataka kuniambia nini usiku wote huu?

Mpepo: Sina muda. Nina safari ya kwenda Rukwa na Luzolo. Tunakwenda kutafuta mali. Nadhani ulimwona jana hapa na tulikaa faragha kwa muda.

***Itaendelea!***

## Ukamataji, Upekuzi na Dhamana ya Polisi—6

**SURA YA TATU**

**KUKATALIWA DHAMANA YA POLISI**

**Kifungu cha 67** cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai kianeleza kwamba. Mtuhumiwa aliye chini ya ulinzi wa polisi anaweza kukataliwa maombi yake ya kutaka apewe dhamana.

Kwa upande mwingine, kifungu hiki kinamtaka afisa wa polisi anayekatalia dhamana ya mtuhumiwa, atoe sababu kwa maandishi zenye hoja za sababu za kumkatali mtuhumiwa maombi ya dhamana.

Lakini endapo sababu ni mtuhumiwa kushindwa kutimiza masharti au anayekataa masharti yaliyowekwa na afisa wa Polisi kabla ya dhamana kutolewa; basi afisa wa Polisi ***atalazimika*** kumfikisha mtuhumiwa mbele ya hakimu wa Mahakama iliyo karibu haraka iwezekanavyo, ili mahakama hiyo imuhudumie kulingana na matakwa ya sheria.

KUFUTWA KWA DHAMANA YA POLISI

Baada ya mtuhumiwa kupewa dhamana ya Polisi na kuwa huru, dhamana hiyo inaweza kufutwa na mkuu wa kituo, chini ya kifungu cha 68 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai. Kutokana na kufutiwa dhamana, mtuhumiwa atakamatwa tena na kuwa chini ya ulinzi wa Polisi. Baadhi ya sababu zinazoweza kusababisha uamuzi wa kumfuta dhamana ni:-

a) Kubainika kwamba anapanga mipango ya kutoroka

b) Kwa makusudi anakiuka au yu karibu kukiuka masharti ya dhamana.

**ADHABU KWA KUKIUKA MASHARTI YA DHAMANA YA POLISI**

Dhamana inayotolewa na polisi, kwa mtuhumiwa anayekubaliwa na kosa la jinai inapaswa kuheshimiwa. ***Kifungu cha 69*** cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai kunatoa adhabu kali, kwa mtuhumiwa na mdhamini au wadhamini wanapokiuka masharti ya dhamana waliyopewa.

Kifungu hicho kinatamka bayana kwamba mtuhumiwa anapokubaliwa dhamana ya polisi na kuwa huru, endapo kwa ***makusudi na bila busara*** anashindwa kuzingatia masharti ya dhamana aliyopewa, mtuhumiwa anakuwa ametenda ***kosa la jinai.*** Kwa sababu hiyo, anawajibika kisheria kuhukumiwa na kupewa adhabu.

Adhabu atakayopewa haitazidi kiwango cha juu ambacho cha adhabu ambayo itatolewa kama atapatikana na hatia na kuhukumiwa kwa kosa ambalo limesababishwa akamatwe na kuzuiliwa kabla hajapewa dhamana.

**MWISHO**

*Inatoka Ukurasa wa 05*

**Takriri**

Mwandishi ametumia takriri ili kuweka msisitizo

mfano shairi la “Kujitawala” (uk 7-8) neno kujitawala limerudiwarudiwa.

**Matumizi ya Taswira**

Mwandishi ametumia taswira nyingi kama vile;

Kimbunga …(uk 1)…..Kuashiria mapinduzi

Kibwangai…(uk 9)….Kuashiria viongozi wasaliti

Nyani…..(uk 9)…….Kuashiria wananchi waliosalitiwa

Chuwi…..(uk 42)…..Kuashiria ukoloni mamboleo, n.k.

**Jina la Kitabu**

Jina la Kitabu Kimbunga halisadifu yale yaliyomo ndani ya kitabu kwa sababu hatuyaoni mageuzi yoyote ambayo anayajadili katika kitabu hiki zaidi ya mashairi ya maadili mema na maonyo ya kimaisha. Asilimia kubwa ya mashairi katika diwani hii yamejadili juu ya maonyo na maadili katika maisha.

**Kufaulu kwa Mwandishi**

**Kimaudhui**

Mwandishi amefaulu;

Ø Kutoa maadili mema na maonyo katika jamii

Ø Kujadili dhamira ya ujenzi wa jamii mpya

Ø Ameonesha mbinu mbalimbali za kufuata ili tufanikiwe katika ujenzi wa jamii mpya

Ø Baadhi ya maadili aliyoyajadili katika diwani hii ameyajadili kidhanifu, ni sawa na yale tunayoyapata makanisani, ambayo yana nafasi ndogo sana katika ujenzi wa jamii mpya

Ø Vile vile amejadili masuala mbalimbali kidhanifu hasa anapomhusisha Mungu. Kama vile masuala ya kipaji (uk 38-39), bahati (uk 36), umaskini (uk 35).

**Kifani**

a) Ametumia lugha rahisi, mafumbo, taswira, n.k.

b) Mwandishi ametumia lahaja ya Unguja badala ya Kiswahili sanifu ivyo ni vigumu kueleweka kwa watu wote.

c) Diwani hii ni ya hali ya chini sana katika muundo, mtindo na baadhi ya vipengele vingine vya kisanaa.

**Mwisho!**



# HADITHI

## RAIS WA CHUO – 02

***Inatoka toleo lililopita…***

“Yes!” Waliagana. Hasheem alishuka garini akarudi hostel. Alipofika chumbani kwake, kabla hajafanya kitu chochote alishtushwa na mvumo mkali wa sauti ya mlango uliokuwa unagongwa kwa fujo. Alivua koti haraka akalitupia kabatini.
“Ramin, ni wewe!” Alisema Hasheem baada ya kuufungua mlango.
“Ni mimi,” Ramin alijibu.
“Vipi! Mbona usiku na hujanipigia simu kama unakuja?” Hasheem aliuliza kwa mashaka.
“Tuingie ndani tafadhali,” alisema Ramin. Aliusukuma mlango akaingia chumbani kwa Hasheem.
“Kuna nini?” Hasheem aliuliza akijaribu kuupima umbali wa mawazo yake na kilichomleta Ramin ghafla namna ile.
“Mbona una wasiwasi sana, kulikoni?” Aliuliza Ramin kwa utulivu huku akimwangalia Hasheem machoni.
“Wasiwasi! Wasiwasi wa nini?” Hasheem alishtuka moyoni. Ujio wa Ramin aliuhisi kuwa tofauti na siku zote. Hakuwahi kumtembelea bila kumuuliza yuko wapi.

Kwa hivi, alihisi huenda ameshtukia jambo la muda mfupi uliopita. Hata hivyo, alijitahidi kukumbuka kama katika harakati zake muda mfupi uliopita ziliweza kuonwa na mtu. Alikumbuka tangu alipopokea simu na kuzungumza kwa muda mfupi kisha naye kupiga kwa mtu mwingine na kuongea kwa muda mfupi pia. Alikumbuka namna alivyotembea kutoka chumbani kwake hadi kwenye gari na alivyorudi. Hakuona mawazoni mwake namna Ramin aliweza kushtukia alichokifanya.

“Hasheem sikuelewi,” Ramin alisema baada ya kuingia chumbani kwa Hasheem na kuhakikisha mlango umefungwa vizuri. Hasheem alishtuka – mshtuko ambao Ramin aliubaini haraka. Moyo wake ulikimbia mbio kwa hofu. Kijasho chembamba kilimtoka. Kwa namna alivyojawa na hofu hakutulia.
“Tulia Hasheem uniambie. Kuna nini?” Ramin alimtuliza.
“Nakuomba tafadhali usimwambie Kanyika, atavunjika moyo,” alisihi Hasheem baada ya kutulia na hofu kumwondoka. Alimuangalia Ramin usoni kama aliyetaka ithibati ya alichomuomba. Akaendelea, “Sina nia mbaya ila nimebananishwa sana. Nimejaribu kuuepuka mtego huu lakini nimenasa.”
“Imekuwaje?” Ramin aliuliza.
“Huu mpango ni mkubwa sana. Yumkini una cheni ndefu. Kuna mkono wa serikali katika huu uchaguzi. Kikubwa Kanyika hatakiwi kuongoza serikali ya wanafunzi,” Hasheem alifafanua. maneno yake yalimchoma Ramin.
“Hawamtaki Kanyika, kwa nini?” Ramin aliuliza katikati ya maumivu yake.
“Tatizo sio Kanyika, tatizo ni mgombea-mwenza, Kikoti. Kikoti ni mpinzani, nadhani unalitambua hilo,” alifafanua Hasheem.
“Nalifahamu. Ni mwenyekiti wetu tawi la chuo,” alijibu Ramin haraka.
“Hapo ndipo penye shida.”
“Kwa hiyo wamepanga kuvuruga uchaguzi?” Ramin aliuliza kwa jazba.
“Ni kuvuruga, in fact. Wanataka kutumia hila kuhakikisha Kituka anakuwa Rais wa chuo bila kujali kura zinatosha ama la.” Kilipita kimya cha muda mfupi. Kisha Hasheem aliendelea, “Wanahitajika vijana hamsini ambao watatumiwa katika hila zao.”
“Umeshawapata?” Ramin aliuliza kwa tafakari ya muda mfupi juu ya jambo hilo.
“Nitalazimika kuwatafuta ingawa nimewaambia hadi kesho watapatikana zaidi ya arobaini na watano.”
“Ok! We’ umeamuaje?”
“Hakika sifurahii!”
“Nani mwingine anajua kuhusu hili?”
“Balonzi.”
“Hawajasema hao watu watawafanya nini?”
“Hapana. Nadhani wanataka kuwapa fedha.”
“Hakuna kilichoharibika. Waache walete hiyo hela halafu sisi wenyewe tutaamua,” alisema Ramin. Hasheem alimgeukia Ramin macho yao yakakutana.
“Unawajua wanaoleta hizo hela?” Aliuliza Hasheem akijaribu kumtahadharisha.
“Yeyote atakayeleta.” Ramin alijiamini.
Bado Hasheem alimwangalia Ramin usoni kama aliyemuonya. Kichwani yalipita maswali mengi kwa mkupuo mmoja lakini swali moja tu lilijirudia mara

nyingi. *Ramin alijuaje kinachoendelea?*

Katika mchakato huu, mtu pekee kuambiwa hatua zote ni Balonzi. Huyo aliambiwa siku ya kwanza kwa kupigiwa simu na hao watu. Hasheem alimfuata ili kumtaka ushauri juu ya ama akakutane nao au la. Balonzi alimshauri akakutane nao lakini akiweka sharti la kufahamishwa kila kitakachojadiliwa. Sasa leo ghafla namna hii Ramin amefahamu kila kitu tena ndani ya muda mfupi tu. Alitaka kumuuliza alivyoujua mchakato huo lakini alitulia hadi wamalize mazungumzo yao.

"Ramin, nihakikishie kwamba hautamwambia Kanyika wala Kikoti jambo hili."
"Kanyika ndiye Rais wa Chuo hiki ndiyo maana wanahangaika. Hawamuwezi kwa hoja na siasa zake. Kwa hiyo, tunachokubaliana mimi na wewe na Balonzi na hao watu hamsini au mia moja, ni kuhakikisha Kanyika anashinda," alisema Ramin. Aliweka msisitizo katika kila neno lake. Hasheem alivuta pumzi ndefu akazibana mapafuni mwake kwa sekunde kadhaa kisha aliziachia.



MAKOLEKO KALIBONGE
o

"Hili jambo unalichukulia kama mchezo wa kuigiza sio?" Alifoka Hasheem.
"Haliwezi kuwa maigizo. Nakuhakikishia watakuja kuharibu taswira ya chuo hiki kwa mambo ya kipuuzi kama haya." Ramin aliwaka. Macho yake makubwa yalizunguka chumbani mule kwa haraka.
"Mambo haya yanapita. Kanyika kutokuwa Rais hakutampunguzia maungo yake." Woga ulimwingia Hasheem. Alijikuta anajuta kujiingiza katika mambo ambayo hayakuelezwa kwenye fomu za kujiunga na chuo. Hofu yake kubwa ilikuwa katika kitakachotokea baada ya mchakato huu. Mipango ya Ramin haikumruhusu kuamini kwamba atakuwa salama iwapo Kanyika atashinda. Alijiona katikati ya watu wanne wenye kuogofya. Atawaambia nini? Alijiuliza.
"Ni kama vile Kituka kutokuwa Rais hakutampunguzia maungo yake," Ramin naye alisema kwa dharau.

"Ok! Ramin. Tusianzishe malumbano yasiyokuwa na tija. Hili jambo mi' binafsi silifurahii na silipendi. Tufanyaje?" Aliuliza Hasheem.
"Niachie mimi. Kukipambazuka nikutanishe na Balonzi kisha nitajadiliana naye. Hao watu hamsini watapatikana na zaidi ikibidi," Ramin alijibu.
"Sawa. Ila lipo jambo moja nataka kulifahamu."
"Jambo lipi?"
"Hili jambo umelijuaje?"
"Ha ha ha ha haaa!" Badala ya kujibu, Ramin aliangua kicheko hata Hasheem naye alicheka.
"Mtu wa mwisho kuzungumza naye ni nani?" Aliuliza Ramin.
"Kwa hiyo, Balonzi ndiye amekuambia?" Hasheem alishtuka.
"Ndiye mtu wa mwisho kuzungumza naye?"
"Ndiyo! Ni yeye," Hasheem alijibu.
"Una uhakika?" Hasheem, badala ya kujibu, alitoa simu yake iliyokuwa mfukoni. Aliangalia mtu wa mwisho kuongea naye. Alipotazama kioo cha simu akatataharuki. Haraka alimgeukia Ramin kisha alitazama tena kwenye simu asiamini alichokiona. Simu ya mwisho aliyoongea nayo ilikuwa namba ya Ramin. Wakati ule alipopokea simu ya wale watu kujulishwa kuwa wamefika naye alitoa simu kumtaarifu Balonzi ambaye alishamwambia ujio wao mapema sana.

"Jamaa wameshafika naenda kukutana nao. Tukutane *room* baada ya muda." Aliyakumbuka na maneno aliyoyasema.
"Kwa hiyo tumeshaelewana?" Aliuliza Hasheem.
"Kwa asilimia mia moja," Ramin alijibu. Waliagana Ramin akaondoka.

❦

Thebby alikaa kushoto na upande wa kulia alikaa Alvie. Katikati yao alikaa Nyambuna. Kawaida yao kila walipokutana hukaa hivi. Nyambuna ni mtu mzima wakati Thebby na Alvie walikuwa wari wadogo wa umri wa kati. Hiyo ndiyo sababu walimwita shangazi kila walipomwona au kuongea naye simuni. Aliwapenda sana kiasi cha kutamani kuwa nao kila mara.

"Shangazi, leo hujaenda kwa mjomba?" Thebby ali-

## RAIS WA CHUO – 02

uliza kwa utani. Badala ya kujibu swali aliloulizwa, Nyambuna alitabasamu. Tabasamu ambalo liliupamba uso wake hata kuonekana mwari wa miaka ishirini na saba ilhali ameshakunja makumi manne na nusu.

"Mjomba wenu amepata likizo," alijibu Nyambuna katikati ya tabasamu lake. Walicheka kwa pamoja wakagongesheana vidali.
"Shangazi!" Aliita Alvie kama aliyetaka kusema jambo na sasa alitaka umakini wake.
"Niambie mwanangu," Nyambuna alimwitikia.
"Nitakuwa First Lady wa chuo very soon," Alvie alisema. Wote kwa pamoja, kama walioambizana, waliangua kicheko.
"Yaani nyie watoto mna mambo kweli," Nyambuna alisema halafu aliuliza, "Na wewe utakuwa nani?" Alimgeukia Thebby.
"Mke wa Waziri Mkuu huitwaje?" Thebby aliuliza.
"Mh!" Nyambuna aliguna. Kimya kilichukua nafasi ya mazungumzo yao japo kwa muda mfupi. Kisha Nyambuna aliuliza, "Hivi, huwa mnawasaidia wenzenu kufanya kampeni?"
"Kusema kweli…" alisema Alvie huku akiuweka mkono begani kwa Nyambuna. Alimgeukia kumwangalia usoni kisha aliendelea,"… mi' na siasa kama usingizi na kitanda chenye kunguni. Sijui tu huwa wanamaanisha nini wakisema siasa."
"Siasa ni mchezo unaochezwa na watu wanaotaka madaraka kwa ajili ya watu wengine." Nyambuna alimuwahi. Kimya kingine kilifuata. Ni kama vile walitaka kuendelea na maongezi yao lakini hakuna aliyetaka kuanzisha maongezi hayo.

"Nimemsikia Kanyika akisema anafikiria kujitoa." Hatimaye Alvie alisema. Nyambuna alishtuka. Aliushika mkono wa Alvie uliokuwa begani akautoa. Alimgeukia akamtazama usoni.
"Unasemaje? Kwa nini ajitoe?" Maswali mfululizo yalimtoka Nyambuna.
"Anasema Kituka anapewa sapoti kubwa na Chuo," alijibu Alvie uso wake ukiwa chini. Furaha iliondoka miongoni mwao.
"Haitoshi kuwa sababu ya kumfanya ajiondoe," alisema Nyambuna kwa masikitiko. Sikitiko lake halikuwa dogo, lilikuwa kubwa kuuzidi ukubwa wenyewe. Katika moyo wake, alimchagua Kanyika kuwa Rais wake. Mara kadhaa alimfanyia kampeni alipokutana na watu alioweza kuwaambia neno wakamuelewa. Taarifa za Alvie zilimvunja moyo. Alitamani siku moja amuone kijana huyo akiwa juu zaidi ya urais wa Chuo. Alipenda namna alivyoweza kujieleza. Aliupenda wepesi wake katika hoja zake. Sasa anataka kujitoa kisa hana sapoti ya Chuo? Ni sapoti gani aliyoihitaji? Alijiuliza.

"Mpigie simu mwambie nataka kukutana naye," alisema Nyambuna. Alvie alichukua simu. Alibonyeza bonyeza kisha aliweka sikioni.
"Kanyika, shangazi anataka kuzungumza na wewe," alisema Alvie akakata simu.

❦

**UCHAGUZI KESHO**

Asubuhi iliyofuata hali ilikuwa shwari. Mlango wa chumba namba 111 katika Block 1 uligongwa. Baada ya sekunde chache ulifunguliwa. Juliana mbele Christopher nyuma waliingia chumbani humo. Chumbani waliwakuta Shafi Kituka na Jonta Nyamwaro wakiwasubiri.
"Kumekuchaje ndugu zangu?" Aliuliza Kituka.
"Na makucha yake!" Alidakia Nyamwaro. Walicheka.
"Enhee! Tunaanzia wapi na tunamalizia wapi?" Kituka aliuliza baada ya kicheko.
"Ratiba inasemaje?" Christopher naye aliuliza.
"Hii hapa," alisema Jonta Nyamwaro akikimbilia mezani haraka na kurudi na karatasi.
"Ni sehemu mbili tu; tunaanza na College of Education kisha tunamalizia uwanja wa nyumbani kwa Wanasheria," alisema Christopher baada ya kuipokea ratiba kutoka kwa Nyamwaro.
"Upande wa pili nao vipi?" Kituka aliuliza tena.
"Ratiba ile iko wapi?" Christopher aliuliza akimgeukia Juliana. Juliana, kwa muda mfupi, aliufikia mkoba wake alioupachika mgongoni. Aliufungua akatoa karatasi.
"Ni kinyume chake – wanaanzia College hii kisha wanaenda kumalizia Education," alisema Juliana akiikunja ile karatasi na kuirudisha mkobani mwake.
"Hii ndiyo fainali ndugu zangu. Ukisikia tonge la mwisho hukomba mboga ndilo hili," alisema Kituka kabla

ya kuendelea, "Leo ndiyo siku ya kumwaga sera zote zilizobaki. Ndiyo siku ya kuhakikisha tunaua upande wote ule asibaki mtu hata mmoja akipumua, labda kwa msaada wa mashine." Kimya kilifuata.

Kila mmoja alizama kwenye tafakuri. Kama alivyosema Kituka, hiyo ilikuwa fainali. Ilikuwa siku ya kuvuna mbivu au mbichi. Siku ya kujua kama watavuna walichostahili au la. Wakati fulani, fikra zilimwambia hii ni vita – ni vita kubwa. Vita iliyohitaji ushindi. Yeyote anaweza kushinda ikiwa amejiandaa vizuri. Na, zaidi ni vita iliyohitaji silaha sio kali tu bali za kisasa.
"Kila kitu kimetayarishwa?" Hatimaye aliuliza Kituka baada ya kimya kirefu.
"Kila kitu kipo mstarini; kuanzia gari la matangazo, watu wa burudani na mabango mapya yanabandikwa kila baada ya dakika kumi," alisema Christopher.
"Vizuri," aliafiki Kituka na kuuliza, "Kuna lolote kutoka kwa Kirusi chako?"
"Mpendae ameshapanga mambo yake tayari," alijibu Christopher.
"Kama ndivyo, tukajiandae kwa ajili ya kumaliza jambo hili," alisema Kituka. Kikao kilivunjwa kila mmoja aliingilia njia yake.

❦

Balonzi aliingia darasani alimozoea kukutana na Hasheem. Lakini alishtuka badala ya kumkuta Hasheem kama walivyofanya alimkuta Ramin amejaa tele. Ilikuwa baada ya kukubaliana kati ya Hasheem na Ramin usiku uliopita kwamba asubuhi inayofuata Ramin akutane na Balonzi. Mshtuko wa Balonzi haukuwa kitu kwa Ramin. alijitahidi kuuficha akidhani Ramin alikuwa na mambo yake na baada ya muda ataondoka.
"Balonzi!" Aliita Ramin.
"Vipi Ramin, mbona asubuhi sana uko humu na uko peke yako?" Balonzi aliuliza. Ramin alikaribia kucheka kwa swali hilo. Alijizuia.
"Njoo tuzungumze ndugu yangu," alisema Ramin akichanua tabasamu. Balonzi alishtuka tena. Mshtuko huo ulimstaajabisha Ramin.
"Ni mambo ya kawaida tu Balonzi, usishtuke." Balonzi kama aliyefumwa na mke wa mtu, alisogea alipoketi Ramin. Naye aliketi.
"Ni mambo ya kawaida tu ndugu yangu yasikushtue," alisema Ramin. Balonzi alitulia.
"Umepata watu wangapi hadi sasa?" Ramin aliuliza. Ungemwona Balonzi alivyoshtuka hungedhani kama alikuwa shababi. Moyo ulimwenda mbio kama aliyefukuzwa. Haraka aliwaza huenda Hasheem alimuuza kwa Ramin juu ya mpango wao. Tamaa ya fedha ilikaribia kumtokea puani. Alijua kama taarifa zimemfikia Ramin zitamfikia Kikoti. Kwa sababu Ramin na Kikoti ni wanachama wa chama pinzani. Mara nyingi wamekuwa wakisuguana katika masuala ya siasa. "Hasheem ni msaliti," alijisemea moyoni.
"Watu wa nini?" Aliuliza badala ya kujibu.
"Balonzi, nafahamu kila kitu. Niambie tu umewapata watu wangapi?" Kama Polisi, Ramin alimkazia macho Balonzi. Balonzi alikwama.
"Mh!" Balonzi aliguna. Kijasho kikamvuja.
"Sikiliza," alisema Ramin. Kisha aliendela, "Hasheem ameniambia kila kitu. Naomba nikuhakikishie na nikutoe wasiwasi, jambo hili hakuna anayelijua zaidi yetu sisi – mimi, wewe na Hasheem. Na, nakuhakikishia pia hakuna atakayejua zaidi yetu sisi labda kama umewambia mtu mwingine."
"Hapana! Sijamwambia mtu," alisema Balonzi akishusha pumzi. Alipuna jasho kwenye paji la uso akasema, "Kanyika hapendwi kwa sababu ya Kikoti. Nadhani unalifahamu hilo."
"Ndiyo. Nalifahamu," alisema Ramin halafu akauliza, "Nawe humpendi pia?" Badala ya kujibu, Balonzi aliinamisha kichwa chini.
Ramin hakumjali. Alijikohoza kidogo kulegeza koo akaendelea, "Ukweli Kanyika anatosha kuwa rais na Kikoti makamu wake. Hawa wanaotaka kufanya jambo hili lengo lao wamuweke Kituka na Nyamwaro. Hii ni serikali ya chuo na mambo yake yanaishia chuoni. Kwa nini watu wa nje ya chuo watuharibie?"
"Hata mimi nimeshangazwa sana," alisema Balonzi.
"Hapa tunakubaliana na tutakachokubaliana ndicho kitakachofanywa. Hao watu wanataka kutuharibia uchaguzi wetu. Tusikubali, " alisema Ramin.
"Tumechelewa Ramin," alisema Balonzi kwa sauti ya chini iliyokata tamaa.
"Hatujachelewa ndiyo maana mwanzo nilikuuliza nani mwingine anajua hili ukasema hakuna zaidi yetu. Si ndio?"
"Ndiyo."bus

Itaendelea toleo lijalo...

**Tangazo**




www.richardmwambe.com

JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com